Com Ahmed Hassan: (inaudible) John Lekodei.

John Lekodei: Asante sana Bwana Chairman maoni yangu si mengi sana. Tunashukuru kwa kuwa mlikuja hapa wale mnasimamia maneno ya Katiba ya Kenya, na kitu ningependa kuwa uliza nyinyi kabla sijaendelea, ninaona tunaongea mambo ya Katiba ya wale wazima pekee yao, kwa sababu kama ingekuwa inaweza kutuwakilisha hata sisi, sababu mimi ninaongea kwa niaba ya wale wajuaji Kenya nzima. Hapa mahali tuko ninaitwa John Lekodei (*in vernacular*), ni Vice Chairman, (?) Marigat, na ninafikiria kabla kutaja maoni yangu ningependa kuwa uliza nyinyi ni Serikali

(inaudible) sababu kama ninavyo elewa...

(Interjection) **Com Nancy Baraza:** Weka Microphone mbele kidogo (inaudible)

John Lekodei: Nafikiria....

Com Ahmed Hassan: Unajua mzee ukiisongesha microphone karibu sana, itaharibu...

John Lekodei: Sasa ninafikiria itakuwa sawa. Nafikiria kama...

(*Noise from the audience*)

John Lekodei: (inaudible) kwa sababu imesemekana sana sana kwa Katiba ya Kenya
(inaudible) kwa sababu maneno mengi (?) tuko wengi sasa hatuwezi hata kuja hapa kutoa maoni yao, yanayo hitajika kusaidia kwa Katiba ya Kenya baadaye.

Ninafikiria sasa, sisi ni watu wale hatujajulikana au tumesahauliwa kwa Katiba, kwa sababu wakati mwangi, tuko na watoto, ni watu tuko na watoto lakini wanasona na hawana watu wanawasimamia hao watoto wao. Mara wanafukuzwa shule, hawana... kama uko na watoto wako kusaidia familia yako nyumbani, nafikiria hata hao watoto wataumia. Na chochote itafutie wale hawajajulikana, mambo ya kazi, na wale wamesoma lakini hawaja pata kazi bado. Pengine hamjaweka

(inaudible) binadamu kama nyinyi.

Ningependa kuwaomba nyinyi mkijenga Kenya, mkiendelea namna hii ni vizuri kwa sababu ukiona sasa hata parliament hakuna (?) huko parliament wanatusaidia sisi, wale hawajiwezi humu Kenya. Hakuna wale ma-Councillors,

(Inaudible) ndio inaweza kuwasaidia hawa, inaweza hata kuwasaidia waweze kujitetea wenyewe kwa wenyewe, isipokuwa parliament wanajitetea. Wakichukua location, wanajitetea. Sasa mambo ya KANU, hakuna watu wanawasaida hawa kujitetea na sisi ni watu tu. Na tuko (?) juu ya kujitetea.

Kwa hivyo ningependa kusema sasa mambo ya hospitali (?) tunaumia sana ndio unaona sababu mimi ninaongea.
Kwa sababu (Inaudible) na nitaongea namna hiyo, tumeumia miaka mingi. Kwa sababu nilikuwa na watoto ninawapeleka hospitali, mimi mwenyewe ninaenda, ninapiga kelele saidia sisi (?) mambo ya Serikali
(inaudible) ndio tunajua sasa ndio watu ni kama nyinyi. Lakini kama nyinyi ndio mliweka kiti kando (?) kwa hiyo sababu sasa kama hiyo (?) tunafikiria hamjamua kama wakati (inaudible)nafikiri huko waliteuliwa watu kama (inaudible) lakini kama nyinyi hamjamua namna hiyo, mtusaidie huyo jamaa, mtusaidie tafadhalii, kwa sababu kuna wale wengine kama hawasimami wana mwakilishi wao kutoka parliament, kutoka KANU kutoka location, division mpaka district lakini (Inaudible) na ninataka mtusaidie sisi kabisa ikiwa na chochote ambacho watu husaidika.

Mambo ya ardhi, pahali pa kuishi. Vile mnavyojua sasa Kenya ni watu

(inaudible) ndipo mnaona sasa sisi mambo ya ardhi ni ngumu. Mahali pa kwisha ndio kama possible mtu mzima anaanza kung'ang'ania. Kama ma plot, huwezi kupata. Mashamba ile watu wanapata huko, hatuwezi kupata kwa sababu hatuna pesa, hatuna wale wanatusimamia sisi kama wawakilishi wetu. Kwa hivyo wangeongea ingejulikana tu kwa hivi kama hatujapata hiyo sababu ya hiki na kile ingetambuliwa tu. Kwa hivyo sasa mimi ninasema (in vernacular).

La pili, nikikaribia ya mwisho, ni kitu ambacho kishasemwa na nilisema hiyo kama (?) hajalipiwa kitu hamgejua. Lakini ya pili mambo ya (?) sasa kama nyinyi wajamaa mnakimbishana huku na huko. Mara kwa upinzani, mara KANU. Je mnajua sisi ni watu hatuna mahali tunaenda, hakuna mahali tunakimbia, tunakaa tu hapo na tunakufa hapo hapo. Kwa hivyo kile kitu ambacho nilikuwa Ninawaambia nyinyi ni kwamba mtusaidie sisi kwa kila jambo. Mambo ya hospitali, mambo ya masomo, kinyumbani. Kwa sababu wengi sasa hawawezi kupata hata ndururu ya kula! Na usifikirie pengine hawatapata mwisho wa mwezi kama vile wengine wanapata pesa lakini mimi sipati kwa sababu hakuna, hakuna kazi mimi niko nayo. Pengine niandikwe kazi kidogo, ingine na watu wawili, watatu. Wengi wao wanaumia nyumbani! Kukaa kwa nyumba.

Kwa hivyo ninafikiria... Nitamaliza kwa kusema mambo ya Constitution. ingawa imesemwa na wale wa mbele, hapo kodi inafaa kupatiwa constituency yao (?)

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** (inaudible)

John Lekodei: Haya sawa sawa. Kwa hivyo ninafikiria kuhusu hiyo constituency, hapa kunaitwa Baringo constituency ingefaa kuwasaidia hawa. Kwa hivyo ninashukuru sana na mambo yetu mchukuwe kwa njia ya inatakikana. Thank you very much.

Com Ahmed Hassan: Bila kupoteza wakati kwa sababu kuna watu wengi tujaribu kuchunga saa ni watu wengi wanataka kuongea
(inaudible). Tupate Julius Lokisoi.

Julius Lokisoi: Bwana Commissioner ninashukuru sana na ninawaunga mkono wale watu wengine amba wameongea.

(interjection) **Com Ahmed Hassan:** Anza na jina lako.

Julius Lokisoi: Mimi ninaitwa Julius Lokisoi. Kile kitu ningependa kuongeza ni kwamba, tusiwe wakimbizi wa hapa Baringo. Vile vile tunesema mmesema mambo mengi na nikipitia hiyo nitachelewa. Ille (?) ilikuwa ni ya watu wengine tangu zamani, ingawa wale walikuwa wenyeji wametosheka nayo.

(inaudible)

Kile kitu kingine ningependa kusema tuko na shida nayo, ni usalalma. Usalama wa (?) ni kidogo sana hapa Baringo. Wa (?) wale wafugaji wa ng'ombe wanakuwa wakasumbuliwa sana kwa vitisho na majirani. Wanakuja wanachukua ng'ombe wao, mtu anauwawa na hatua ya kweli haichukuliwa. Unakuta pengine kama polisi anapelekwa wanenda kuchunga ma-refugee badala wafuate wale wamewasumbua hawa. Na stesheni za polisi hakuna ambayo inasimama katikakati ya mji huu ambayo inachukuliwa hatua kwa haraka. Ukingalia hii (?) ni sehemu ndogo sana ambayo haiwezi kutumaniwa usalama na hawa watu wote (?) unaona? Zile shule zingine wa Njemps wako nayo.

Barabara, communication, barabara ya lami inaishia hapa Marigat na ku-divert kuelekea huko (?) ambayo sasa kama huko barabara ime-cross hapa katikati ya Uasin Gishu mpaka itoke Samburu, ingekuwa (inaudible) mngekuwa na biashara nyingine tofauti na communication ingekuwa rahisi. Kama upande wa Samburu ndio kuna biashara mzuri tungkuwa tuna communicate nao. Lakini sasa Mnjemps akitaka kwenda Samburu mpaka apande gari ya kuelekeza Nakuru halafu aeleke (?) huko lakini njia ya hapa ni usalama hakuna.

Kwa hivyo, lile lingine ningesema, tunataka utawala. Sisi tutawale tukiwa Wanjemps wa hapa ambapo sasa kama Wanjemps zamani wangkuwa na mtu mwakilishi katika bunge ingekuwa rahisi (?) kufika pale. Lakini kwa sababu tulikuwa tunatawaliwa na kiongozi wa nje ambaye yuko busy wakati wote, sio rahisi kufikia, unasikia mtu mwingine ndio Wanjemps wamechelewa kimaendeleo mpaka sasa.

Promotion; Wanjemps tena wale wanasoma, mtu anakalia promotion moja miaka kumi, miaka mingine kumi na mitano kwa sababu ya njia (?) ya kupenya au kupita ama kuendelea na masomo mengine ya kuongeza ni shida; kwa sababu

hakuna mwakilishi katika bunge, unaona. Wengine wameshindwa kusoma kwa sababu ya ukosefu wa bursaries, na hivi vitu vingine vya kutusaidia na mashule mengine kama yale ya watu wakubwa wakubwa (?) waone? Tena utawaonesha hiyo ma plot? Wanjamps haushiwi kwa hiyo kugawanya ardhi yao. Unakuta wengine wanakuja na mali kutoka sehemu zingine wanasema plot hapa, na pale na pale pengine ni ya fulani. Hakuna Mnjemps ambaye anaelewa. Kwa hivyo hiyo tunasema tunataka constituency ya Wanjamps na hiyo ni Mnjemps mwenyewe anaongoza. Yangu ni hayo, asante sana.

Com Ahmed Hassan: (inaudible). Raymond R Kipkorir, yuko? Kama hayuko Ezekiel (?).

Ezekiel Parkena: Nafikiri kabla hatujaongea, ningepongeza kamati hii ambayo imekuja kusikiliza maoni ya kutengeneza Katiba mpya. Basi mimi ninawaunga mkono wale wenzangu ambao wamezungumza kuhusu constituency. Mimi ni Ezekiel Parkena, vile umenitaja hapo. Nafikiri ninaunga mkono vile wenzangu wamezungumza juu ya constituency.

Kwa kusema ukweli, sisi tumewakilishwa kwa muda na Mtukufu Rais na tulifurahia uwakilishi wake. Na vile sasa tulikuwa watu wachache hatungeweza kutosha tumtoe mwakilishi wetu, lakini kwa wakati huu sasa nafikiri tumeweza kufika kiwango cha kuweza kutoa mwakilishi wetu. Nafikiri ninaunga tu mkono hiyo, hiyo nafikiri mtachukua kwa roho mzuri.

Kuna jambo lingine ambalo ningependa kuongeza. Ningependa kuongeza juu ya elimu.

Elimu nafikiri pande kubwa, kwetu hapa kuna ukavu sana. Kuna watu wengi wameshindwa kuwaelimisha watoto kwa sababu ya ukame ambao umewakumba. Unajua sana, sana upande hii wanategemea wanyama, na kuna wakati wanyama wao wanakwisha kwa sababu ya ukame, na hapo sasa tunakosa namna ya kuelimisha watoto.

Tena kuna kitu kingine ningependa kuongeza tena. Ni juu ya afya, health. Hata sasa tunashida sana. Ukipatwa na ugonjwa unaweza kufa na huo ugonjwa, kwa kuwa huna kitu cha kugharamia matibabu hospitalini. Na hapa sasa madawa yamekuwa ghali sana hata mwananchi wa kawaida hawezi kujimudu kujilipia gharama ya hospitali. Kwa hivyo ninaomba Serikali iangalia mambo ya hospitali, waweze kutoa huduma hiyo kwa bure.

Vile, vile juu ya mambo ya biashara. Kutembea ndio kitu kinacho weza kuwasaidia wananchi. Hapo tunaona mambo ya biashara yako chini sana, kwa kuwa sisi ni watu ambao tunategemea wanyama, na hatujawekewa soko la kuweza kuwauza hawa wanyama wetu ili tuweze kujisaidia maishani. Kwa hivyo ninaomba Serikali ituangalie mahali pa soko ya wanyama hawa kama KMC, au mahali ambapo tunaweza kujisaidia kwa wanyama kama hawa. Nafikiri hiyo ndio ingetusaidia maishani tuweze kusomesha watoto, ama mambo ya kugharamia matibabu hospitalini vile nilikuwa ninasema. Basi ninafikiri hivyo ndio tunaweza kusaidika. Kwa hivyo ninaomba Serikali yetu ituangalia kwa mambo kama hayo.

Kuna tena mambo ya maji. Hapa kwetu hatuna maji safi ya kutumia. Kama vile kuna dam moja ambayo iko hapa Chemeron,

hiyo dam imejengwa tu ya maji na tunayatumia hayo maji

(?) Hatujapatiwa namna ya kutunza hayo maji ili yawe safi

kwa kutumia. Tunaomba Serikali ituangalia kwa hali ya maji ili tupate maji safi ya kunywa. Nafikiri bila kupoteza au kuchukua nafasi nyingine mrefu, yangu ninafikisha hapa. Asante.

Com Ahmed Hassan: Asante sana. Samson Lekakimol.

Samson Lekakimol: Honourable commissioners, my names are Samson Lekakimol.

(Interjection) **Com Nancy Baraza:** Lekakimole?

Samson Lekakimol: Lekakimol. I am a student at Egerton University. I wish to first of all express my gratitude for your coming especially to Marigat for this particular mission. I think it is very important and it is our hope that our views will be expressed in the current new constitution. So we have some few expectations that vary in this new Constitution.

We feel that the forth-coming general election should be held under a new constitution. This is just to create a level playing ground, so that democracy can take place. It is our hope again that under the new Constitution, our views will be accommodated because us being a majority and (?) immediately we felt that the old constitution was not containing any views that is to our interest.

I would like to talk about national resources especially issues concerning lease of land. I am talking a lot because I am a lawyer by profession, and I stand to be corrected if anything. There are issues, this is to do with the lease that last ninety nine years (99) and other places where you talk of this lease lasting for about 33 years. I am of the view that this one should be cancelled, and should be debated especially agreed upon by the parties concerned. That is now to pave way for the people to manage their land. On the same point, our Land Bill that is now coming under the trustees land, should again have a board regulating them. This board should be elected where we talk of... we can consider gender that is in this case the (?) representation. This one will now assist such that this land will not again fall under Local associations.

I would again want to talk about the issue of governance. I am of the view that there should be separation of powers where we have the President, the Prime Minister who is in charge of the government. Now, we should openly have the Central system of governance or political system where we talk of majimbo.

Now here, I would once again talk about the qualifications. For one to be the President, he should be a graduate, just the same way as the MPs, for you to be an MP you have to be a graduate. Coming to the Local authorities, the qualifications there, should be Form IV and above.

We should again talk of education where if being a disadvantaged group, that is the Njemps. The Njemps being a disadvantaged group and particularly a clever lot of the side of agreement of 1904 and 1911. This agreement brought a lot of problem that is in Laikipia side such that we were displaced where we are. Our time here...

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** (inaudible)

Samson Lekakimol: 1904 and 1911, this (?) That is to pave way for the white settlers in Laikipia.

I am of the view that our children or rather this land should return back to the people that is the Njemps. They should be given this land and if it is not possible that they should be given this land, then our Children should learn free of charge. Education needs to be free that is on the (?)

I have also talked on nomination. The nomination, we lack recognition that is the current constitution...

(Interjection) **Com Nancy Baraza:** Sorry, spell for me Njemps.

Samson Lekakimol: Njemps.

Com Ahmed Hassan: Go ahead, go on.

Samson Lekakimol: So I would like to correct again that tribe because I am talking about recognition. You are now calling us the Njemps. We are not the Njemps we are the (?) and we are saying the current Constitution is really giving us little recognition in that line. If you have seen the Daily Nation of 18 June 2002, where the MPs are literary campaigning, one of our old men was photographed and given a different name altogether. So in other words we are not recognized.

So in that light, I would want the new Constitution to give special recognition especially the minority groups, or the disadvantaged groups of Kenya on that particular matter. Otherwise thanks a lot for that opportunity.

Com Ahmed Hassan: Thank you. Please sign the register. Simeon Oletengech?

Simeon Oletengech: First of all commissioners, I just want to take this chance to say thank you for taking a second opportunity in Marigat to air our views as a community in this important occasion that you set aside. Well, I just want to give my few suggestions that will include some two items...

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Start with your name.

Simeon Oletengech: My name is Simeon Ole Tengech. Well, the Njemps community concurs with the rest of Kenyans in recognizing the need for the review of the current constitution. The Njemps community is a Maa speaking group occupying Marigat, Mokitany and recently the new Mochongoi division of the larger Baringo District. We want to correct this anomaly about the word Njemps. This word has been particularly disturbing to us but coming up to the root of this community because there is no evidence of Njemps. We are the Il-chamus

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Can you spell the word.

Simeon Oletengech: Il-chamus. This was prescribed by the colonialists because of illiteracy. There was nobody to write these names correctly and pronunciation we believe caused this anomaly.

Com Ahmed Hassan: Okay, go on.

Simeon Oletengech: The name Baringo is derived from the Il-chamus word Mparinko and is referred to the current lake Baringo. The historical, religious and economic activities think of the Ilchamus community revolve around lake Baringo, and they have great attachment to the lake. Mparinko is spelt M p a r i n k o.

Originally the Njemps community occupied the land, an extension of the Laikipia Plateau to the East to the (?) to the West. Likewise from the Northern source of lake Baringo to the Northern source of Lake Bogoria known by Il-chamus as Mpatipat.

(interjection) **Com Ahmed Hassan:** Spell it.

Simeon Oletengech: S m p (for Peter) a t i t a t, Smpatitat. The Il-chamus center and language are completely different even from the two current tribes Tugen and Pokot in Baringo District while the larger part was the community is conveniently pastoral in nature, they also practice subsistence agriculture and fishing.

Land and Natural Resources: Land is a (?) for any community and to the Njemps, it is just more than that. Land is seen as a cultural hold, the identity and their way of life. The Njemps consider themselves as the custodians of the earth, rather than owners. They are custodians of their land which all the stages have to come and they have been bound with their culture, spirit, identity and survival. Without land registry their culture the Njemps will not survive neither have identity.

Trust Lands Act: The ownership of land, Mr. Chairman as is basically inform of land which is as a form of ownership is qualified in the sense of not being direct owners by the Njemps themselves. As a result the (inaudible)

from the Central Government, the County council and other
through a
(?)

(inaudible) this qualification of ownership

(inaudible) of their right of ownership of land and constitute

Current seminars and recommendations: The majority of the Njemps in view of the current constitution, they were not aware of their rights because of illiteracy and because of poverty they were not able to excel to understand or be aware of what is there. Then we have had various anomalies in it and there have been various problems in it. This means that the rights

(Inaudible) of the community are either misrepresented or not represented at all. Due to the land tenancy

(inaudible) the community has lost land, and it continues to lose much of it. Land to merchants who do not respect the symbolism.

The average Njemps initial poverty levels have continued to rise thereby retarding development. In this aspect we want the review constitution to recommend to
(?) for the Njemps community or for the community.

The infrastructure of the Njemps people: poor infrastructure in the area has come in front of several other things. They understand
(inaudible) this has denied the community the opportunity to eradicate illiteracy. So we want the Review Commission to recommend that the groups be equipped by giving them teachers. The government to see the places which teachers are not adequately edited and...

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** One minute left, try and summarize.

Simeon Oletengech: The Commission proposal: The Njemps community like their own competition un-met and they did not want to really recognize that it is coming from such a minority community
(inaudible) in Kenya. Recognize that the rich and the unique culture of the Njemps people is fast disappearing due to rising poverty levels. Recognize their past encroachment of their native land and therefore provide mechanisms for these people. Protect the community from possible split of their
(inaudible) without public and a written context and a
(inaudible) we all own that one block within one constituency.

Provide for the right of constituency and representation
(inaudible) in parliament on the strength of the fact that Njemps are indigenous minority strengthened by mis-interpretation. Provide for a law to conserve the environment within the main settlement areas for the lake Baringo
(inaudible) that is Laikipia
(?) and Mau escarpments because that is where these rivers which are the
(?) of these communities well being is seen to degenerate and the community is actually going to have a problem in the future.

Lake Baringo being an important natural resource for the Njemps community should be protected and a law be enacted to

safeguard it...

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Summarize eh.

Simeon Oletengech: Yea, and a law enacted to defend it. Provide for the (?) of the Kenyan (?) of private land ownership because the thing is communal ownership of land is not helping much and that is why there is a lot of encroachment and that is why there is environmental degradation and so many other things in that state. So it is our wish that in the county council who are practicing the

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** I have told you for the third time please summarize. Your time is up, you have finished your time.

Simeon Oletengech: To summarize, I just want to say that the County Council who are the trustees of these lands and the community. We don't have... we need these constitution to recommend in such a way that what they amend it, let everyone

(inaudible) and as a community we only have three people who will represent us in this (?) and we wanted this issue of land, that if I happen to (?) kwa hivyo people are (inaudible) ministry of local Government then there (inaudible). Thank you.

Com Ahmed Hassan: Thank you. Sasa, I want to make one request. I have said this in the morning, but then I think some of you have come late. Wengine wenu mlikuja mwisho baada ya kikao kuanza. Kama uko na maandishi kama huyu mwenzetu Simeon, we are requesting, please do not read it word for word, the way he was doing it. if you can try and highlight the main points, yale maneno muhimu. Usijaribu kuisoma neno kwa neno, kwa sababu hiyo itachukua muda mrefu. Kwa hivyo tunawataka please, mjaribu kuchukua yale maneno muhimu halafu mnayataja.

Com Nancy Baraza: Niko na swali kidogo. Ninataka tu nipate clarification au ufahamu, kwa sababu kila mahali tunaenda Wakenya wanasema tunataka tribe yetu iwe kwa Constitution, tu recognize in the Constitution. Sasa nyinyi tuseme nyinyi ni Il-chamus or Il-njamus?

Response from the audience: Il-chamus.

Com Nancy Baraza: Kwa sababu tunaweza kuandika Il-chamu, mseme hao ni watu wengine si Njemps, ndio tunataka tujue nyinyi ni kina nani.

Response from the audience: Il-chamus.

Com Mohammed Swazuri: Tungependa kusema leo ni (?) Kenya nzima. Kwanza hiyo constitution review ambayo ilikuja ni mbaya sana. na tungependa iandikwe tumekuta atu wanaitwa Il-chamus.

Com Ahmed Hassan: Ni kweli hiyo?

Response from the audience: Ndio.

Com Mohammed Swazuri: Na kama jina Il-chamus wale wote wa lugha hiyo ningependa wasimame na waseme asante.

(Interjection) **Com Nancy Baraza:** Weka mikono juu tuone lift up.

Com Ahmed Hassan: Haya sawa tumeona. Paul Kanyaman Lemigure?

Paul Kanyaman Lemigure: Asante sana mwenyekiti.

Com Ahmed Hassan: Majina yako?

Paul Kanyaman Lemigure: Majina yangu ninaitwa Paul Kanyaman Lemigure, kutoka (?) Mimi ninaongea tu maneno matatu. La kwanza ningetaka kusema ninaunga mkono wale watu ambao wameongea kwa ajili ya kuomba kuwakilisha Baringo kwa sababu ukiwa na mzee ambaye una vijana kama watatu ama wanne, kijana wa kwanza akiwa mkubwa, hamwezi kuishi pamoja; kwa hivyo mimi ninaomba hiyo ikiwa mtu wa community ya Njemps ama community ya Njemps yote kwa jumla, kwamba nimekuwa kijana ambaye ninaweza kujisimamia ama nimekuwa mkubwa nikaomba baba nijenge kwangu.

La pili ningesema hivi, mimi ni mtu ambaye niko na miaka hamsini na sita. Na sasa wakati mzee, mtukufu Rais, nilikuwa kabisa kwenye mji wakati ambao alikuwa anaongea akisema atawasimamia. Nasiwezi kuwadanganya hawa vijana, ninasema haki. Mpaka wa leo hatuna ubaya na mzee. Ni wakati wake umefika, ama kama bado anaweza kuwasimamia, Wakenya wanapenda awasimamie, bado tuko na yeye. Lakini akiwa amechoka ama ametaka kwenda kusimama, tunasema ya kwamba hakuna mwengine atawasimamia. Nina vijana ambao wamesoma, wamepata masomo ya kutosha. Kuna vijana wako Masters, vijana wa degree, diplomas. Hata kwanza tukiwa sasa jinsi hii hakuna mwalimu tunatumia Primary anakaa nami hapa, (?) pekee yake.

Kwa hivyo hayo tu ndio mimi nitasema. Na ninasema, nyinyi sasa mko wageni hapa. mko watano. Na mimi nikiwa mbunge wenu au mkubwa wenu, na mlinichagua na niseme wale wasichana hawawezi kuniona; na nyinyi watu watatu wanania. Wale watafurahia mimi? Basi hayo ndio maoni yangu.

Com Ahmed Hassan: Asante sana, enda uandikishe jina lako huko nyuma. Antony Lodopich.

Antony Lodopich: Asante. Ninasema asante sana kwa Commissioner. Ninashukuru Commission hii kwa kufika hapa, ili tuweze kutatua neno kama hili. Mimi ninaitwa Antony Lodopich kutoka Njemps. Mimi ningependa kushukuru commission kwa sababu ninataka kuchangia vile wenzangu walisema. Kwa sababu kwetu tumeongea zaidi ya kwamba, mtoto ukizaa hutawacha tu acae hivyo bila kupea mali, na kama umekubali kuzaa, lazima upeane mali kwa mtoto wako ili aende ajitegeme. Kwa hivyo tunashukuru

(?) kwa kusema ya kwamba, sisi kama Njemps tungependa kabisa kwa sababu baba yetu atapumzika, na kama amekubali kwenda kupumzika, nimesema asante kwa sababu ametufanyia mengi. Na sisi tunaomba kwa Serikali, sio kwa nguvu; ya kwamba sisi tutambuliwe kama jamii nyingine. Tupewe nafasi yetu ya kujisaidia.

Pili ni mambo kama hii ya mahospitali. Kweli, wananchi wote wanateseka sio sisi Njemps pekee yake hasa (?) kwa sababu tunapata kama mahali inatiwa dispensary, kwa dakika hii sio ajabu kuambiwa nilipe shilingi mia mbili, ili upate dawa ya kutosha ili mtoto wako apone. Na hiyo shilingi mia mbili hata shilingi kumi ni ngumu ile ya kununua kadi ya hospitali. Tungependa matibabu hospitalini ipeanwe free, kama vile ilikuweko zamani, ili watu wapate kujisaidia.

Mambo mengine ni kama hii ya County Council. Hapo zamani wakati tulikuwa wadogo, mambo yakifanyiwa kwa Council yanafika kwa mwananchi, kama mambo ya land. Unakuta kama mimi nimekuwa nikikaa kwa hii ploti, unakuta hiyo ploti imepewa mtu ambaye yuko Nairobi kwa sababu yeye yuko na nguvu. Nikijaribu kulalamika ninaenda kortini. Hayo mambo ya kuenda kortini ninaomba Serikali ya kwamba kama ni mambo ya ardhi sisi tuje tuongee kama jamii ya hapa hapa, ili tutatue mambo ya ardhi. Kwa sababu kama nilivyokubali wote tuende kortini huenda matajiri watafaidika kwa sababu watakuwa na nguvu.

Lingine ni mambo ya hawa wazee ambao wanaitwa elders, ambao ni wazee wa kijiji. Serikali ingeangalia sisi (inaudible) hawa wazee wanasaidia watu sana kijijini, kwa sababu vita vya usiku, vita vya nini, hatuwezi kufika kwa chifu kwa haraka, tunawaita hawa headmen anawasaidia watu hapa. Kwa hivyo tungeomba kabisa, Serikali iwafikirie hawa watu wanaitwa headmen, wapewe nafasi.

Nitaenda kwa mambo ya elimu. Hiyo ninataka kuchangia kwa upande wa nursery schools. Sote tungetaka tuwe sawa Kenya nzima msingi yote ni nursery schools. Ni ajabu ya kwamba waalimu wa nursery school wanapelekwa training tunasikia huyo mtoto ako na certificate (?) unaambiwa ni wakati wa lipe nursery school dible), ni ajabu. Na yeye ni mwalimu kama wengine. Kwa hivyo tungependa kabisa hawa (inaudible) mtu aliye sisi wananchi kwa sababu tuko hapa kwa semi-arid, zile mahali mbaya, mbaya sana sio town, watu wengi hawana kazi. Kwa hivyo tungependa hiyo tusaidiwe, hayo mambo ya nursery schools.

Tunakosa kazi hasi sisi community ya Njemps, tuko na matatizo mingi. Kweli vile tunajua kwa sababu tunataka mbunge (inaudible). Unakuta majina yameletwa kitambo, unasikia mtu ameandikwa na mimi ninafanya hii kazi (?) kwa nini sikuambiwa nikae nyumbani niende nipumzike? Unakuta mtu ameandikwa kwa kazi kama Jeshi na army. Watu wachache wanaleta watu waokitambo (inaudible) na kama tungekuwa (?) tunaambiwa tuje karibu tungelalamika kwanza lakini sasa saa hii tunalalamikia na nani? Tuko na Councillor lakini Councillor nguvu yake inafikia hapa na kurudi nyuma. Kwa hivyo tungependa sisi vitu kabla hiyo, tuangaliwe.

Pia mambo ya maji, kwetu tuko na maji ya kutosha kama hii Pekera. Lakini hii Pekera kwanzia sasa sisi tukiwa kutoka jamii kabilia tatu hapa, kama Pokot, Tugen na Njemps, haya maji yameanza kutumiwa kutoka huko kwetu. Pekera haikuwa hivi, hii Pekera ilikuwa kubwa. (inaudible) kwa hivyo tungeomba wale wako na nguvu watupe maji tafadhalii iende chini kwa sababu tumeteseka kwa sababu ya maji. Kujaribu kuongea hakuna nafasi. Kwa hivyo tungeomba kitu kama hiyo. Ile dam kama hiyo ya Kolon, hiyo dam iko na maji chafu sana, na hayo maji yanaenda mpaka mahali panaitwa (?) nafikiri kama (?) kuna mahali inaitwa (?) Primary School, hiyo maji inakuja mpaka huko.

Na hayo maji ni chafu kwa watoto, ukikunywa unapata typhoid. Kwa hivyo tunaomba Serikali itusaidie sisi kwa upande wa maji. Watutafutie sisi maji yale safi ili watoto wetu wapate maji safi. Watoto si wa Njemps pekee yake lakini ni wa kenya nzima. Kwa hivyo tusaidiwe na mambo ya maji.

Barabara: Kwetu hatujasaidiwa na barabara. Iko barabara ya kwetu inaenda mpaka Laikipia. Hiyo barabara saa hii ukitembea hapa hata kama una (?) siku tatu, mbaya na watu (?). Kwa hivyo tungesaidiwa kwa mambo haya ya barabara. Watu ambao wanahuksika na mambo ya barabaran watutengenezee sisi barabaran ili communication yetu iwe karibu na (?) kwa hivyo asanteni sana, yangu ni hayo tu.

Com Ahmed Hassan: Asante. Laban Boiwo.

Laban Boiwo: Mimi ningetaka niongee kuhusu mambo ya Katiba. Ningetaka niwashukuru nyinyi ma-Commissioner, ambao mmeufika hapa siku ya leo ili kupata mambo kutoka kwa wananchi. Ya kwanza ningetaka niseme Bwana Commissioner ni kwamba, haya mambo ya Commission yametufikia sisi kwa upande wa kushoto, hayatukujia kwa mkono wa kulia. Sababu ya kusema hivi ni kwa sababu, sisi kama wananchi hatujui hata Constitution Review ya kwanza, Constitution ile independent iko aje. Hata ukimuuliza mwananchi, Constitution number moja ni nini hajui. Sisi tunajua tu Section 2A ile ilikuwa repealed huko Parliament hata mtu hajui.

Kwa hivyo kama wananchi tungefundishwa Constitution kutoka moja hadi mia moja sijui na ngapi, na tuambiwe siku ya leo

tubadilishe, tungekuwa na nafasi nzuri ya kubadilisha hii Constitution. Wale ninaamini wanajua pengine ni wale mawakili na wale wamesoma mambo ya sheria. Sisi wengine hatujui. Kwa hivyo tutafanya yale tunajua, lakini kama ingekuwa maoni yangu, hii Constitution Review wangepewa muda wa kutosha, wafundishe wananchi, wananchi waelewe halafu wabadirishie Katiba kulingana na matakwa yao.

La pili, ningependa kuongea kuhusu mambo ya Judiciary. Mimi kwa niaba yangu ninataka niseme haya mambo ya kortini yamekuwa na matatizo sana. Utakuta mtu anafanya makosa, akifika kortini anatakikana ushahidi, shahidi atatwa apelekwe mpaka Kabarnet, mwananchi hana pesa ya kumpeleka huyo shahidi. Huyo shahidi akifikishwa huko Kabarnet anakuwa frustrated mpaka watu wameogopa kutoa ushahidi. Serikali itafute namna nyingine ya kuchukua ushahidi kwa wananchi kwa njia nyingie kuliko kutaabisha mwananchi kwa kumpeleka safari ya mbali. Ama korti iletwe karibu na wananchi, ili mwananchi apate kutoa maoni yake kwa kweli.

Siku hizi kuna watu wamekuwa wajeuri zaidi, ninaweza kuwaita pengine ma-jailbirds. Hao wamesomea mambo ya korti, wakifika huko wana frustrate efforts zako zote, anasema urongo mpaka inaonekana ni kweli na inakubaliwa na judge anathibitisha kwamba huyu mtu hakufanya makosa. Lakini kwao mwenyewe ameona ni makosa lakini kwa sababu ya sheria ambayo iko, sio nzuri, inafunga mtu ambaye hakufanya makosa. Na yule mwenye kufanya makosa, anaachiliwa. Hayo ndio maoni yangu kuhusu mambo ya Judiciary.

Nikiingia upande mwingine, nitaongea kuhusu mambo ya irrigation rule. Haya mambo ya irrigation rule, ningeomba kama ingewezekana ifanyiwe overhaul! Mwananchi anakubaliwa kuwa chairman miaka yote, (inaudible) na kunyang'anywa hiyo shamba, hana mahali pengine pa kwenda kwa sababu pengine National Irrigation Board wako na title deed ama ni Serikali. Kama ingewezekana mwananchi apewe kibali akikaa na hiyo shamba na ajue ni yake, na afanye matumizi na maendeleo ndani ya hiyo shamba akijua ni yake.

Lingine ni kuhusu mambo ya machief. Chiefs wapewe jukumu kiasi ambayo wanaweza ku-control mwananchi katika location. Ma-chief wakiwa hapa ni (?) ya location, wamekuwa frustrated anatusiwa (?) hata na mwananchi, hata hana mwelekeo. Hawezi kumsaidia mwananchi, kazi yake itakuwa ni bure! Sasa tutaendelea kuishi maisha ya aina gani? Tutaishi namna hii kwa muda gani?

Lile lingine ni African marriage. Tunataka ieleweke na ihalalishwe na Serikali, African marriage iwe na kibali kama zile zingine. Kwa sababu unakuta wazee wengine wana oa bibi kwa African marriage, halafu wanaenda wanoa bibi mwingine kikanisa, ama anaoa kwa D.C. Yule wa kwanza hajulikani, amepotea huko msituni. Kwa hivyo ningeomba Serikali ipeane cheti kwa kina mama wale wameolewa nyumbani, hata hao wajulikane.

Lingine ni kuhusu mambo ya school fees ambayo watu wamesema. Ninaunga mkono kwamba shule kutoka darasa la kwanza

ama kutoka nursery mpaka Form IV iwe bure, ili kila mtu apate ku-participate. University iwe mtu anaweza kulipa, aende sasa kusoma huko. Na kama inawezekana sisi wananchi wote, Kenya nzima kama tutapatiwa tax ya kwamba kila mtu aweke shilingi tano, tano ili mtoto aende shule. Kila mtoto aende shule, kila mtoto afike Form IV. Hiyo itakuwa tunasaidika watu wa Kenya.

Lingine ambalo ningetaka kuongea juu yake ni kuhusu mambo ya Local Government. Local Government wamepewa uwezo

(?) ma-Councillors. Kiwango kwamba ikiwa sikupigia Councillor kura, huwezi kupewa ploti. Akisimama huko Kabarnet aone jina langu anakata. Kuwepo na utaratibu ambao kila mtu ako na haki ya kupewa plot, uwe umempigia mtu kura au haukumpigia. Sio kwamba Council wa decide kwa sababu Councillor hanipendi mimi, wanaita jina ama wanafanya nini, akisikie jina langu anakata. Council haina utaratibu wa kupeana maploti, kwa sababu ma-Councillors pekee yao ndio wanatawala hizi ploti na wale watu hawakumpigia kura wanaumia miaka yote. Hawatapata ploti...

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** La mwisho.

Laban Boiwo: Lile la mwisho, ni kuhusu mambo ya elections. Elections ziwe zinafanywa na secret ballot kwa sababu nimeona ya kwamba kina mama wanakosana na wazee wao kwa sababu mzee anataka mama ampigie fulani kura, na ameona fulani ameweka mlolongo kumpigia mwingine kura. Haya mambo ya mlolongo yawe abolished. Iwe ni KANU au opposition sote tuwe wangwana ndio haki itendeke.

La mwisho ningependa kuongea kuhusu mambo ya ugawaji wa ardhi. Watu ambao wanapata mashamba utakuta ni watu ambao wako na mashamba. Wale watu ambao wanaitwa landless hawawezi kupata shamba. Kwa hivyo tutafute namna kabisa ya kuona ya kwamba yule mtu anapewa shamba ambaye ni landless awe kweli ni landless. Ikiwa mtu anatolewa kutoka mlima ule anapelekwa mlima ule mwingine. Mosop aingie mpaka Mosop ingine, hawa watu wa kwenu wote hawana chochote, wamekauka, na wanaendelea kukauka. Kwa hivyo itafutwe namna ambayo wale ambao kweli ni landless wawe settled.

Lingine ni kuhusu haya mambo ya plot. Tafadhali ningeomba mambo ya Commissioner of Lands iwe abolished kwa sababu wale werevu wanaenda kwa Commissioner of Lands, wana-grub Marigat yote, sisi wenyeji tukienda huko kwa Commissioner of Lands, tukitaka kuomba plot, hakuna plot. Ni plot ya fulani, plot ya fulani, kwa sababu hao wanajulikana. Kwa hivyo haya mambo ya Commissioner of Lands, yawe abolished, wananchi wawe na uwezo wa kutatua mambo ya mashamba yao. Asanteni.

Com Ahmed Hassan: Samson Kimutai.

Samson Kimutai: Asante sana Commissioners, kwa kututembelea hapa Marigat. Ninayo maoni machache sana na ningependa kuyasema kwa ufupi. Katiba mpya, ningependa wananchi ama kimila iingize kwa vile unawenza kuta kama sisi

Kalenjin. Kuna vitu vingi ambavyo unakuta kwa ndani inatumika kwa ile Katiba ya kwanza, hii ambayo ni ya Lancaster House ile unaona kuna zingine (?) kwa hivyo ningeomba tuhusihswe ama tupewe nafasi kwa Katiba hii mpya.

Nikichukua mfano, tuseme sasa kama kuna Katiba inasema kwamba, gari ikikanyaga ng'ombe, unakuta mwananchi yule hana kitu chochote anaambiwa alipe gari ya millioni tatu. Unakuta sasa hapo mwananchi anaumia sana. Kwa hivyo ningeomba Katiba itungwe ya kulinda hata mwananchi kwa mali yake, kama hiyo gari.

Nikienda kwa upande wa Councils. Ningeomba, ama ningependelea mayor wa jiji achaguliwe na wananchi sio Councillors peke yao. Lingine ni kwamba kuna nominated Councillors ama nominated MPs. Hawa mimi ningeonelea kwamba kama ingewezekana wasikuweko, kwa sababu sioni kile wanatekeleza zaidi kupita yule amechaguliwa na wananchi.

Jambo lingine ni kuhusu administration. Ningependa Katiba iundwe ya kwamba machifu wawe wakichaguliwa na raia wenyewe. Sio kwamba wanaenda kwa interview maana siku hizi kumetokea hii mambo ya corruption. Unaweza kuta mtu ana apply kuwa chifu halafu anafuatilia kupeana kitu kidogo huko, ili apewe awe chifu. Kwa hivyo ningependelea kwamba chifu atoke kwa wananchi wenyewe, kama vile ilikuweko hapo mbeleni.

Nyingine ni mambo ya elimu. Mambo ya elimu ningependelea Constitution iunge ya kuwa watoto wasome bila kulipa chochote vile wenzangu wamesema. Mengine ni kwamba nilisikia mwenzangu hapa akisema ya kwamba hawajui sheria ya ukweli, hawakufahamishwa. Kwa hivyo ningeomba Constitutional Review wakubali tuendelee kufunzwa Civic Education, ili wajue mambo ya sheria.

Jambo lingine ningependa kusema ni kwamba uchaguzi ujao. Sheria mpya itumike kwa uchaguzi ujao. Ya mwisho ni kwamba ningependa Katiba iandikwe kwa kila lugha. Maana kuna wazee hawajui kwa Kiswahili sasa ikitembelewa Katiba number one inasema hivi kwa Kiswahili, hawaelewi. Kwa hivyo ningeomba Commissioners wachukue hilo jambo. Kwamba Constitution iandikwe kwa lugha zote. Kwa hayo machache asanteni.

Com Ahmed Hassan: Asante. Dickson Chepkut. Samson Kimutai, please sign the register huko.

Dickson Chepkuto: Vile iko kwa Katiba, sisi hatuko (inaudible) kwa sababu ni (?) katika Constitution hii. Tukp na walimu (inaudible) hatujui sababu na ni Serikali ilisema watu wafunge (?) sasa sisi hatujui kitu cha kusema kwa sababu (?)

(Interjection) **Com Nancy Baraza:** Ni Chepkut or Chepkuto?

Dickson Chepkuto: Chepkuto.

Com Nancy Baraza: Wacha tu nikwambie, labda hukupata Civic Education kwa ule muda mngependelea lakini tungetaka Wakenya waongee maneno, yale maneno ya day to day life, yale yanawahusu kila siku. Ongea yale maneno ya moyo. Kama wewe ni mnani? Il-chamus?

Dickson Chepkuto: No.

Com Nancy Baraza: Kalenjin?

Dickson Chepkuto: Mimi ni Tugen.

Com Nancy Baraza: Tugen, eh. Ongea maneno ambayo yanakuhusu, ya kila siku. Usiseme hauna cha kusema. Kwa sababu hata kama haujui ile Constitution ile tuko nayo na mimi ni mwanasheria, lakini hata mimi sielewi hiyo Katiba. Nisikudanganye, hatuelewsi sana. Ni Katiba ambayo wazungu waliotengeneza na ni ngumu. Sasa usiseme hauna cha kusema. Toa maneno ambayo yanakuhusu, kwa vile unaishi na vile ungetaka uishi na utakuwa na kitu cha kusema.

Dickson Chepkuto: Sawa, (inaudible) sasa sisi watu wa (?) na hatukusema, tuliuliza (?) kwa County Council tuende kortini. Kuenda kortini hawa wakatusukuma sisi nje kwa sababu hawa ni (?) Sasa kile kitu mimi nilikuwa ninaona, sisi turudishiwe Lake Bogoria kama wale wengine kama Maasaini.

Pili, watoto wetu wasome kutoka huku kwa sababu hiyo lake (inaudible) sisi watoto wetu kutoka nursery school kama ingefaa. (?) Neno lingine ni kuhusu ma chief. Kwa maoni yangu hata ma chief wapigwe transfer... (*Laughing from the audience*) kwa sababu...

(interjection) **Com Ahmed Hassan:** Tunyamaze tafadhali, tukitoka hapa Marigat, tutakuwa tumechukua tu ule mcheko wenu, mnacheka na kupiga makofi. Tafadhali tunyamaze kwa kuwa hiki kitu kina-record hapa.

Dickson Chepkuto: Kwa sababu ma chief (*end of tape*) sasa ingetosha kama wangepigwa transfer (?) mtu wa Mandera akuje hapa hajui kitu. Kama upande wa town watu wengine wamekaa kama askari, wanatoka kwao wanaenda North Eastern, wa North Eastern anakuja hapa, itakuwa vizuri kama Councillor, Councillor ni mzuri kwa sababu baada ya miaka tano wanaenda. Kama chief anaweza kaa hii miaka yote atakaa tu.

Neno lingine ni kuhusu mashamba na mwenzangu alikuwa amesema. Mtu anatoka highland yuko na shamba, lakini watu wa hapa hakuna shamba. Tunajua hapo town (?) Mochongoi ilikuwa ofisi yetu, Mochongoi Location, na saa hii watu wa Mochongoi labda ni watu watano wako na mashamba. Kwa nini na hii ni location yetu ikapewa watu? Ipewe mtu wa Nakuru,

mtu wa town na sisi wenyiji hatuna shamba?

Neno lingine... natukienda kuuliza unaambiwa hakuna shamba, na ukienda kesho huko unakuta mahali uliacha jana iko watu. Tungepewa hiyo shamba watu wa low land kwa sababu hata mtu wa highland akiletwa aishi hapa kama ni Baringo. Ataishi kweli?

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Lingine?

Dickson Chepkuto: Lingine ni kuhusu headmen, wazee wa kijiji.

(inaudible) Serikali ingeangalia welfare ya sub

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Wanaitwa nani?

Dickson Chepkuto: Chepkuto.

Com Ahmed Hassan: Hapana, hawa wazee wa kijiji wanaitwa nani?

Dickson Chepkuto: Sub-headmen.

Com Nancy Baraza: Sema hiyo jina.

Com Ahmed Hassan: Sebedmen?

Speaker: (From the Audience): Sub-headmen.

Com Ahmed Hassan: Oh, sub-headmen? Endelea.

Dickson Chepkuto: Serikali ingeangalia welfare yao, kwa sababu ni hawa tuko nao usiku na mchana. Hata ukiwa kwa shamba tuko nao tuseme chief atakuja kama imeisha...

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Tumesikia hiyo, tumejua. Jaribu kumaliza.

Dickson Chepkuto: Kufikia hapo sina neno lingine.

Com Ahmed Hassan: Asante, enda u-sign huko kwa register. Olempaka Amos.

Olempaka Amos: Kwa majina ni Olempaka Amos na niko na haya ya kusema (?) na ule upande wa elimu, education. Mimi ninaonelea kuwa katika nchi hii au (?) pahali ambapo tuko, ikiwa ni Njemps tuko na mashule chache sana na tunataka watoto wasome. Katika hali hiyo, mimi ninaonelea kuwa Serikali inafaa waongeze shule nyingi katika eneo hili. Mashule haya yawe yatagawanishwa, wasichana wawe upande wao, na vijana wawe upande wao. Kwa sababu tunaona sisi wenyeve hatuna wasichana ambao wamesoma tu na tunataka kuelimisha wasichana, gender equality.

Lingine ni upande wa elimu tena, tukifikisha tu kwa hiyo (?) Vijana hawa ambao wanamaliza mashule hapa, huwa wengi wao wanateseka kwa sababu ya ukosefu wa kazi, employment. Tunaona kuwa vijana hawa wanatoka shule, kufikia hapo hakuna mali nyingi. Tunauza ng'ombe ng'ombe. Tunaweza kuja tunasimashwa kazi nyumbani saa hizi sisi ni watu ambao tunaweza kufanya biashara, self-employed lakini hatuna pesa za kuweza kuendeleza biashara hizo. Mimi ninaonelea kuwa kama serikali inakuja kutuona, wasaidie ili pesa zikuje tundeleze biashara ya kuuza ng'ombe kwa sababu (inaudible). Unaona hata (inaudible) watu wengine wanakuja kununua ng'ombe ambazo (inaudible) inasaidia watoto wengine wakiwa shule.

Nikija kwa upande wa land distribution of power, employment. Mimi ninaonelea vijana ili wapate kazi zaidi, watu wasiwe na madaraka zaidi ya moja katika Kenya. Utaona mtu mmoja anaweza kuwa na madaraka karibu ishirini au kumi. Mwingine anaitwa chairman mwingine ako na cheo hii na sisi ambao tumesoma hakuna kazi na tunataka kazi ziwe distributed fairly.

Lingine ninakuja upande wa community, culture. Culture ni kitu cha maana sana. Tunasema kwa upande wa msingi ya cultural affairs. Tunataka cultural ioneckane. Na tukitaka culture ioneckane sisi Wanjemps tunataka kuenda (?) ili hata sisi tuonyeshe kitamaduni kama Wamaasai na jamii zingine ambao tunataka kuonyesha watu (?). Mimi nikiwa kijana sasa kuna vitu vingine ni mimi nimejaribu (?) siwezi kujua kwa sababu nimeadikimika hapo awali. Tunaona sura ya kitamaduni hapo awali. Na culture hii iwe wazee (inaudible) kwanzia wale wameizoea wajue culture (inaudible) imekuwa directed kwa upande wa (inaudible).

Nikija kwa upande wa economy. Sisi ni watu wa nyama kama vile nilikuwa nimesema . Katika hali hii tunaona kuwa tunakuwa watu ambao tunategemea wanyama sana, na kiangazi inaweza kuja na kuwachukua wanyama. Sasa kama inakaa serikali haikuji kuangalia kwa upande (?) ya wanyama. Wanyama hawa wakifa wataleta (inaudible). Kama juzi wanyama waliisha, na watu wengi walikuwa kwa shida kwa sababu hatuna lingine la kufanya. Kwa hivyo serikali wakuje waangalie watu ambao ni pastoralists. Wanyama wakiisha watafanya nini kwa sababu hii shida ni nature imesababisha kwa kuwachukua wanyama.

Ninakuja kwa development. Development mnasikia nikisema sana lakini (?) kuna mashule hapa ambayo ni ya secondary. Ni ajabu kuwa kuna jamii ambazo saa hizi wanatumia pressure lamp na ni shule ambayo iko katika eneo hii.

Hakuna watoto kuumia na kupata shida ya macho, wanaenda kwa daktari wanatumia pesa nyingi. Tena ukiangalia (?) iko remote sana (inaudible) watoto wako mbali, communication ni mbaya, barabara ni mbaya huwa ninajiliza (?). Tena ukijaribu kuangalia uchumi ile communication (inaudible) ni ngumu hakuna ku-communicate kwa sababu hakuna simu na watoto hawa wako na shida kama hii. Kwa hayo yote sina kitu kingine kipyä.

Com Ahmed Hassan: Enda huko nyuma uandikishe jina lako tafadhali. Lengaka Javan.

Lengaka Javan: Asanteni, kwa majina ninaitwa Javan Lengaka, ninatoka sehemu za (?) Sasa mimi nimekuja hapa kuchangia...

(Interjection) **Com Nancy Baraza:** Weka microphone mbali kidogo.

Lengaka Javan: Nimekuja kuchangia yale ambayo ninaweza kuchangia (inaudible). La kwanza ninachangia mambo ya administration kwangu mimi ninaonelea kitambo kidogo niliona watu kama chiefs amba walikuwa na uwezo fulani lakini baada ya zile powers zao kudidimishwa, administration ikaanza kuwa haina nguvu zaidi. Chief anaweza kutukanwa anyhowly lakini kwa haya yote (?) watoe rules ama ule utaratubu tulikuwa nao hapo awali, maanake wao ndio wako na wale watu nyumbani. So wao ndio wanaweza kupata masilahi na first hand information on problems.

La pili, ninaonelea kwangu mimi kuna miradi fulani Serikali inaweza kuanzisha. Kwa mfano wanaweza kuanzisha miradi kama kuwa na division mahali fulani, lakini it is just a perfect division hatuoni maendeleo katika ile division. For example poor means of transport and communication, hata wale maofisa amba wamestahili kuwa ile division hawaonekani. Hatujui Serikali inafanya nini, na wameamua kuweka ile division ile wananchi waweze kufaidika na hata wapate mwelekeo mzuri.

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Lingine?

Lengaka Javan: Lingine pia, mambo ya education especially sisi na wale ma tribes wako hapa lowland, sisi ni watu wakufuga mali, na wengi wetu tuna ng'ombe, mbuzi na kondoo. So, hatuna mashamba ambayo tunasema totalima saa hizi, baada ya mwaka huu tutapata mavunao mazuri tuuze watoto waende shule au tufungue biashara zingine, la. Basi tunategemea ile mali, na we have the natural disasters for instance drought, ama kiangazi, ikija, tunapata shida sana. Mwaka uliopita unaweza kuona kuwa wanafunzi wengi walitoka shule. Wale wazazi amba hawakujimudu na mifugo ambayo walikuwa wanategemea, wengi wao walitoka shule, ama waliacha shule wakaenda kukaa chini.

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Sasa Unaonelea tufanye nini?

Lengaka Javan: Ninaonelea ikiwezekana Serikali iwauzie mazao yao na hata waweze kuangalia hizi tribes ambazo ziko lowlands, ambao hawana tegemeo lolote. For example watoe mashamba, sio ati wanatoa mtu from the highlands wanampelekea ile highland ingine kumpea shamba na kuna wale wana-suffer, are we not Kenyans? Hiyo ni mbaya sana.

Lingine...

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** La mwisho.

La nne, kuna mambo mengine, yanatakikana, mzee ikiwa mama amekosa na unamchapa ye ye, mama anakupeleka polisi na unaingia taabani, na ukiwa na makosa utashindwa wewe. Jaji hata anaweza kukufunga kwa mwaka mmoja, ama miezi sita,

ama miaka miwili. Mzee yuko ndani sasa mama wa

(?) Kwa sehemu kama hizi zetu, inaweza kugawanya

mtu na bibi yake kabisa; kwa sababu mzee akifungwa, akirudi ataishi na huyo mama tena? Tunaona hiyo ni kitu kingine ambacho anaweza kugawanya manyumba ambayo watu hawataki. Kwa hivyo tunaangalia hata hayo. Kusema kweli tunajua mama ndiye mwenye, anaharibu kidogo kidogo, kwa sababu mimi ninaweza kumchapa, lakini siwezi kumchapa kusema ati ninamuua. Ninamchapa ili aache mambo alifanya, ajue hiyo ni sheria...

(Interjection) **Com Nancy Baraza:** Na yule anakuchapa wewe je?

(Laughing from the audience)

Marko Marutich: Ndio wakati hamsikizani fimbo haikatai kufika mahali popote. Ikiwa mzee umechapwa, na mama amechapwa, lakini tutarudi kusema lakini unajua nani alikuwa mwenye makosa? Hapo atajua mambo hayakuwa mazuri, hata wewe mwenyewe utaenda kwako ukijua hiyo haikuwa vizuri. Kwa hivyo hiyo itachunga boma. Unajua boma, ni lazima mzee ndiye anawachapa watoto, anamchapa mama, na watu wanakaa kwa njia mzuri.

(Laughing from the audience)

La tano...

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Jaribu kumaliza.

Marko Marutich: Eeh, itakwisha tu. La tano, kuna mambo mengine yanasema mkikosana na mama, kile mtafanya kiko kwa mama tu. Unajua mama wakiwa kwa boma ni watu wakutawanya. Kuna mambo mengine ukikosana na mama, kama umemchapa ama mmekosana akarudi, baadaye anasema mimi nimeaachana na huyu mzee. Kufika pale kuna mama anasema ati mali inatawanywa. Mpaka tunaacha ng'ombe iko kwa boma, mbuzi, hata mpaka mabakuli na masahani jikoni. Tukiachwa hivyo sio vizuri. Kama mama anakasirika anaenda kwao halafu tunaenda (?) anarudi lakini kugawanya mali, ati mama anaenda na mali ingine... kwetu sisi tunanunua. Kwetu sisi pande hii ,mali yetu ni ng'ombe, huyo mama alikuta ng'ombe iko boma hiyo. Kwa hivyo sijui inaweza kuja namna gani tugawe hii mali, na mama anaenda kuishi huko na mali ingine, na mimi ninaishi hapa na mali ingine. Hapo tunaona hiyo ni kutawanya maboma ya watu. Kwa hivyo tunadhania iwe mama tu, wale tunagawia pale ni wale watoto, sio mimi na mama, tunagawia watoto.

Lingine kuna mambo inasemekana

(?) kwetu sisi pande hii. Hapo kuna watu wanatugawanya, kwa sababu wakati huu tunasomesha vijana, na tunasomesha wasichana. Wote pengine wamebarikiwa, bado bwana yuko na kazi, na bibi yuko na kazi. Hawa wanachokoza kwa sababu kila mmoja analeta mali. Lakini kwa sisi pande hii wate au wanyama, ng'ombe ile iko kwa boma, ni ile ilikuwa ya babu yangu ndio mpaka saa hii kila mtu anachunga lakini hakuna saa tunasema tunagawanya.

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Umemaliza?

Marko Marutich: Niko karibu kumaliza. Kuna mambo mengine kuhusu watoto tena. Sisi kwa wasichana, tunazaa wasichana tukitarajia wataolewa. Ile shamba iko boma hii, tunawagawia vijana. Lakini labda kwa bahati mbaya iko msichana wangu ambaye bado hajaolewa, ako na haki ya kugawiwa shamba. Lakini wale wanaolewa, hawatapata shamba hapa, labda pengine kama hakuna vijana. Lakini hiyo ni pengine, kama sijazaa vijana, na niko na wasichana pekee ambao hawaajaolewa, wataridhi mali yangu. Kwa hivyo ninafikiri yangu ni hayo tu.

(Clarification) **Com Mohammed Swazuri:** Mzee kwa kimila yenu wanawake ukiwapa shamba kama wako na watoto (?) na watoto ama wanabaki kwa bwana hata wale wadogo wachanga?

Marko Marutich: Eh watachukua tu, halafu wakiwa wakubwa kidogo, wanarudi wanakuja kwa baba.

Com Mohammed Swazuri: Wanarudishwa?

Marko Marutich: Wanarudishwa.

Com Mohammed Swazuri: Na nani? Kwa nini?

Marko Marutich: Kwa sababu unajua sisi hapa tunanunua, unanunua bibi hata huyo bibi ukimwacha mpaka aolewe na mwingine, wale watoto anazaa wote watarudi kwa boma hii. Kama ni bibi nilikuwa nimeoa...

(Interjection) **Com Mohammed Swazuri:** Hata akiolewa na mtu mwingine?

Marko Marutich: Ehe, hata akiolewa na mtu mwingine bahati yangu mbaya. Ukioa yule bibi na ametolewa ng'ombe, watoto wote watarudi kwa boma hiyo ya ng'ombe.

Com Mohammed Swazuri: Na huyu mama kama umemfukuza yeye, na watoto umewachukua na yeye anarudi kwao, atakuwa na haki ya kuridhi ardhi ya babake?

Marko Marutich: Hiyo sasa inategemea, ndio nilikuwa ninasema kama kuna mtoto yule hajaolewa. Lakini kama huyo ambaye amezaa kwangu na ako na watoto wangu...

(Interjection) **Com Mohammed Swazuri:** NI lazima arudi nyumbani?

Marko Marutich: Hakuna anakuja tu kwa hao watoto. Unajua hata wewe unazaa mpaka unazeekea, inakuwa watoto ndio wanatawala boma, wanaleta mama yao akuje kutawala.

Com Mohammed Swazuri: Huo ni mkosi mbaya sana kwa wanawake, kwa sababu amekaa na wewe hiyo miaka yote, amezaa watoto na wewe, sasa utamwambia yeze atoke awasindikishe hao watoto bila mali?

Marko Marutich: Unajua huko kutoa mama, watoto labda ni yeze mwenyewe anakuwa na mambo mengi. Sio lazima utoe bibi yako aende akakae nyumbani mpaka (?)

Com Mohammed Swazuri: Na huyo (?) atakaa wapi?

Marko Marutich: Hata wengine wanaweza kukaa kama kijana wangu amejenga huko na (?) wanakaa na mama yake.

Com Mohammed Swazuri: Mzee asante sana.

Com Ahmed Hassan: (inaudible) hayuko. John Olepaturir? Wesley Cheptum?

Wesley Cheptum: Asante sana. Nimeshukuru kwenu nyinyi kwa kuleta Katiba kwa wananchi wa Baringo. Watu wa Baringo upande huu (inaudible). Tulikuwa tunasikia Katiba iko njiani lakini (?) kuna mambo fulani.

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Sema jina lako kwanza.

Wesley Cheptum: Jina langu ni Wesley Cheptum.

Com Ahmed Hassan: (inaudible).

Wesley Cheptum: Kwa hivyo tunashukuru kwa sababu Katiba imekuja pande hii ya Baringo. Tulikuwa tunesikia Katiba imekwisha lakini (?) pande hii kuna kasoro fulani. Wakati mmoja ofisa wenu wa katiba (inaudible) alihusisha viongozi (?). Tukafunzwa na baadaye wakati aliporudi watu walikuwa wanataka kujaribu (inaudible). Kwa hivyo tunasema pole kwa sababu unajua Katiba ni ya wananchi na (inaudible). Kwa hivyo kama nyinyi (inaudible).

Maoni yangu ya kwanza ningeomba tu kabisa mahali popote Kenya hii kuwe na sheria ya (?) Katiba iwafunzwe kwa watu kwa sababu hiyo ni haki yao. La pili, hapo mbeleni kidogo, ilikuwa mtu kama hapiti mahali, na amezaa mtoto wako mahali, huyo mtoto alishika kipande hapo. Lakini kufikia saa hii, sijui ni Katiba ya saa hii inaleta, au ni Katiba ya wakati wa mbele kidogo na hatujaua ni gani. Kufikia saa hii, mtoto ikiwa amezaliwa hapa na amehitumu miaka kumi na minane anahitaji kupatiwa kipande. Asisumbuliwe kwa kuambiwa kuwa mama yake aliquwa hajazaliwa hapa na kuwa baba yake hakuzaliwa hapa, ati ni lazima aende mahali baba yake alizaliwa. Imagine (?) mpaka Lodwar aende kutafuta kipande. Na huyo mtu wakati hajapata pesa za kwenda mpaka Lodwar anaweza kuenda hapa Nakuru, apate kipande huko ama Kitale, na amefukuzwa hapa. Sijui sasa kama Katiba ya Nakuru ni tofauti, au ni sawa na Katiba ya hapa Marigat. Kwa sababu kuna watu (inaudible).

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Jaribu kutoa mapendekezo.

Wesley Cheptum: Basi nilikuwa ninataka tu haki ya huyo mtu itimizwe. Kama yuko Marigat apate kipande hapa Marigat kwa sababu hapa ndipo mahali alizaliwa.

La pili ningeomba tena Serikali iangalia maneno ya hospitali kwa sababu siku hizi ukienda hospitali kama hakuna pesa (?) wewe unarudishwa (?) mnarudishwa nyumbani kwa sababu hakuna pesa. Na yule mtu akienda (?) ya private, ya mtu binafsi, anaweza kuongea na (?) apatiwe dawa (?) unaambiwa hata uende mbali, unaona sasa huyo mtu ametibiwa ameenda.

Com Ahmed Hassan: Unataka nini? Usiende kwa story nyingi, peana mapendekezo mzee.

Wesley Cheptum: La tatu, tungeomba kabisa, kuwa machief wapigiwe kura kwa sababu mtu akipigiwa kurakama miaka mitano anaweza (inaudible) lakini (?) anaweza kuwanyanayasa watu kama vile ye ye anataka. Kwa hivyo ningeomba kabisa chief apigiwe kura.

Com Ahmed Hassan: Sawa, moja tu.

Wesley Cheptum: Ndio, imebaki. La nne, ni uandikishaji wa kazi kwetu, iko shida. Mtu yule hana pesa ya kuhongana, hawesi kupata kazi na kama inawezekana, Serikali itupilie mbali hayo mambo ya kuhongana; kwa sababu wale hawana pesa hawawezi kuona pesa maishani mwao na no haki yake (inaudible) huyo mtu ataumia hivyo. Na hiyo mambo kama hiyo Serikali iangalie.

La tano, Kenya inatangaza, inasemekana Katiba (inaudible) hata maendeleo hatuwezi kuendelea mbele kwa sababu ya ukabila ule uko Baringo. Wewe ukisimamia kitu fulani, lazima nichunguze kwanza wewe ni mtu wa wapi.

Kama wewe sio mtu wa hapa, unasumbuliwa
wote

(Inaudible).

(inaudible). Hata kama utafanya nini, isemekane watu
wote

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Mzee wacha

(?) kama una chochote sema. Jaribu kutoa maoni.

Wesley Cheptum:

(inaudible).

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Umemaliza? Jaribu kumaliza, la mwisho eh.

Wesley Cheptum: La mwisho tungeomba tu, kama nyinyi ni wajenzi wa Katiba, tafuteni namna Katiba itamfikia kila mtu, kwa sababu kila mtu atapata haki yake. Kwa hivyo yangu ni hayo tu.

Com Ahmed Hassan: Councillor William Kiplagat.

Cllr William Kiplagat: Asante sana Commissioners. Kwa majina ni Councillor William Kiplagat. Yangu ni kwamba ningependa mashamba hii ya group ranches, yaondolewe, ili Wakenya wawe na shamba zao na kuweza kupata haki ya kumiliki. Vile vile Serikali isibadilishe ama kuchukua shamba la mtu yeyote, kwa njia yoyote ile. Vile vile, ile shamba ambayo ingefaa kuwa kwa kila mtu ni kama acre hamsini. Wanaume na wanawake wawe na haki ya kumiliki mashamba. Wakenya wawe na haki ya kumiliki shamba mahali popote nchini Kenya.

Kuna shida tena ambayo tungependa iangaliwe. Wasichana huwa wanatungwa mimba, na tunataka kusema kama ingewezekana mtu akimtunga mimba mtoto wa mtu, aweze kumlisha mpaka awe na mmiaka kumi na minane, au akishindwa afungwe miaka kumi na minane.

(Laughing from the audience)

Halafu chiefs and assistant chiefs wapigiwwe kura na wananchi. Halafu mayor na wenyekiti wa County Council wachaguliwe na wananchi moja kwa moja. D.C. asiwe nominated Councillor.

Maplots ambayo yanapeanawa isimamiwe na kamati ya ile centre
mwingilio wowote ule. Kwa hivyo kamati itengwe kama ni center ya Marigat, hiyo ni center ya kila mahali. Kwa hivyo na
assistant chiefs na kamati wawe wanatengewa ili waweze kutujulisha haki.

(?) ambayo inapeanwa, ili kusiwe na

Kwa mambo ya mishahara ya wajumbe na madiwani, kuwe na tume ambayo itakuwa ikishughulikia mishahara ya Wajumbe na
madiwani. Na madiwani pia wawe wakilipwa kutoka kwa account ile ya wajumbe amba wanalipwa. Halafu pia madiwani

waweze kuongezwa pesa vizuri, ili waweze kuwasaidia wananchi vizuri. Na kukiweko na mambo ya (?) ugawaji wa sehemu ya Ubunge tuhusishe viongozi wote hata kwa (?) Ma-locations yasiwe yana gawanywa mara mbili. Iwe kama ni location, inaenda mahali pamoja yote na isiwe inakatwa halafu unagawa hapa na pale.

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Jaribu kuharakisha mzee.

Cllr William Kiplagat: Ninasema tuseme sasa kama Baringo Central inataka kuwa kama (?) Sasa inaweza kufika location mmoja inagawanywa mpaka (?)

Na vile vile mambo ya elimu. Ingefaa Serikali itoe elimu ya bure kutoka nursery mpaka Form IV level. Halafu kwa university, Serikali iwapatie bursary wale ambao hawajivezi. Hii budget ya Serikali ipewe kama ni pesa ya huduma yoyote ile, iwe inatolewa ifike kwa district, iende kwa division, location, mpaka kwa sub-location; ili iweze kutumikia wananchi kamili.

Com Nancy Baraza: Budget au (?)

Cllr William Kiplagat: Pes kama ya agriculture, kwa sababu hata hapa kwa sub-location iko kazi ambayo inatakikana kufanyiwa kama mmomonyoko na mambo mengine. Kwa sababu unaweza kuwekewa pesa ya agriculture lakini inakwishia huko huko tu. Haiwezi hata kupitia kwa ground ya mwananchi. Kwa hivyo inafaa itengewe inakuja mpaka divisional level, mpaka location, na hata sub-locational level. Hiyo mwananchi aweze kupata hii pesa (?) kwa sababu yeye ndio anatoa kodi.

Nikija kwa mambo ya mabarabara, kuwe na kamati ya watu wa sehemu ambazo watu watafaidika sehemu hiyo. Halafu kama iko pesa (?) ya barabara ni hao wananchi wenyewe wanasimamia hiyo pesa, na kuhakikisha hiyo pesa imefanya kazi; kwa sababu unaweza kuta trekta inapita na inaandikwa elfu kumi imekwisha na mwananchi apite.

Com Ahmed Hassan: Jaribu (inaudible).

Cllr William Kiplagat: Inatakikana kwamba police waongezewe mshahara, ili wasijihushe na mambo ya corruption. Kwa sababu utakuta polisi anaambiwa achunge mamilioni ya pesa, ili hali yeye anapata mshahara wa elfu tatu. Akiona hiyo pesa nydingi atajihuisha na corruption. Kwa hivyo police waangaliwe, wapewe mshahara mzuri, kwa sababu wanachungwa Serikali.

Wale ambao wanaoana kwa kinyumbani, wapatiwe certificate kwa sababu watu wengi huoana kinyumbani. Ikifanyika kwamba mtu amekufa, kupata hiyo inakuwa ni ngumu. Kwa hivyo kama iko jambo ambalo limekuwa likifanywa (?) yaani kama ile certificates zinapeanawa kama zile certificates za kuoana . Chief awe nayo halafu zinasaaida wananchi.

Com Ahmed Hassan: La mwisho?

Cllr William Kiplagat: La mwisho ni kama (inaudible) kama president anakuwa wa mahali kuwe na mjumbe ambaye anachaguliwa. President asiwe mjumbe awe president pekee yake. Na nchi hii kuwe na kiti cha Waziri Mkuu na nchi iwe wa majimbo ambayo kila mahali itakuwa ikijisimamia kwa mamboyao. Asanteni sana.

Com Ahmed Hassan: Thank you very much. Ningetaka kuwatambua wale viongozi ambao wamejuinga nasi, Bwana D.C wa Baringo pamoja na Bwana (?) Karibuni kwa hiki kikao, na wale representatives wengine ambao wamekuja nao. (inaudible) kwa hivyo tafadhalii mjaribu kuangalia time. Kila mtu achukue dakika tano. Charles K Lobatian? Dickson? (?) hawako? Caroline Kiptum?

Caroline Kiptum: I am Caroline Kiptum, I am a freelance journalist. I work for the (inaudible) women. I would like the government to make it possible for the mentally disabled especially the women. They should be taken to hospital, they should be the responsibility of the government, and also their children they should have free education. If not free education, they should be given first priority (inaudible).

Also hospitals should be taken to district hospitals, for these people there are few hospitals for the mentally disabled people, it is only Mathare and the situation there is not good. They should be taken to homes, and be taken care of by Social Workers. And also after being discharged from the hospital, there should be a follow-up to know how they are fairing and also their children need counselling because they are traumatized. Anybody raping or torturing them, should be prosecuted.

I will also talk about land. No one should own more than one hundred acres of land in our country. No doctor working in the government should own a private clinic. The Constitution should live up to its word. Parliament should not be extended. Our law states that the term is five years, and in case of war maybe it can be extended, but our country has no war.

About accidents, drug abuse in our country is very rampant so people who (?) people's lives, may be drivers, PSV drivers, the police, the doctors they should be taken for drug tests. That is why there are many police shoot-outs, this is because of drugs. Also the drivers, we have been seeing our PSV drivers, even smoking bhang when driving. So they should be taken for drug tests. It should be a law, because accidents are rampant in our country.

About cattle rustling; it is seen as a traditional thing, but now it has gone beyond that because the rustlers come, kill, torture people. They even kill women, children... that means it has gone beyond cattle rustling. It should be taken seriously.

The Kenyan people also should know the Constitution. This may protect us from torture, and it will reduce corruption. When

you know you are right, you will never be corrupt; because you will know that if you have done any wrong, and if you go to before a court, you will be protected, you may be jailed for a month or so. But if you do not know your rights you will think that maybe you are going in for ten years, and then you will have to chota kitu kidogo. Thank you.

Com Ahmed Hassan: Thank you very much Caroline Kiptum. David Kamar.

David Kamar: *Kongoi missing.*

Translator: Huyu mzee anasema asante sana.

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Mwambie aseme jina lake.

Translator: Yeye anaitwa David Kamar.

David Kamar: *Kamakingen kiiaketukul amune sikebwā vu.*

Translator: Kwa kusema kweli tulipofika hapa hatukuwa tunaelewa tunakuja nini.

David Kamar: *Kimenye reserve ineni komakimuch kenai akobo konetisvetab CKRC.*

Translator: Kwa vile tuko reserve, na hatujafikiwa na mafunzo haya ya CKRC.

David Kamar: *Ngangololi angololi kouye kaketebi sait kitikin kityo.*

Translator: Hivi ninaongea ninaongea sawa na kitu (2) sisi tulisikia kwa muda kidogo.

David Kamar: *Ngotkekerto bet ak keruive kemboi.*

Translator: Ikiwa mchana tutakuwa tukiangalia na usiku tutalaala.

David Kamar: Amune asikelechech aqchek hijkah Chomus kerubet?

Translator: Anasema sisi Waniemps tunaambiwa lala na imekuwa mchana. Ni kwanini tunaambiwa lala na imekuwa mchana?

David Kamar: *Kotkelechin inye mumut konyek kokertoi biikalak koibabai?*

Translator: Tukiwa kama saa hii tunaangaliana namna hii, na unaambiwa huyu mwingine wewe funga macho, na wewe unaangalia utafurahia?

David Kamar: *Kimoche chitnyo neindoiwech eng Bunge.*

Translator: Yeve anasema tunataka mwakilishi wetu katika bunge.

David Kamar: *Kimoche kandoindet nyo.*

Translator: Tunataka mwakilishi.

David Kamar: *Ndamuchi ait olindo.*

Translator: Kwa sababu kama mungekuwa na uwezo wa kuweza kufika mahali panaitwa (inaudible)

David Kamar: *Ndongololi amite olindo.*

Translator: Ningekuwa ninazungumza kutoka hapo.

David Kamar: *Moroisi ikuiye kieamwoe.*

Translator: Huoni jina iliyoko hapo.

David Kamar: *Amungamua amiyu....*

Translator: Kwa sababu nikizungumza nikiwa hapa...

David Kamar: *Omuchi obwat ole akenuki.*

Translator: Labda mtasema ninasema uongo.

David Kamar: *Tomokero acheck chitnyo nebo Bunge kongete kenyoru Uhuru.*

Translator: Anasema Ilchamus inaitwa (?) huko. Hawajaona mbunge tangu Kenya ipate uhuru mpaka wa leo. Hatujaona mbunge akija kusimama hapo.

David Kamar: *Akoi rani.*

Translator: Mpaka wa leo.

David Kamar: *Komosta neiimikekei....*

Translator: Na sehemu ambayo zinashida...

David Kamar: *Ak kemwoei kelen kitinye chito nemi Bunge?*

Translator: Na hivyo ndio mnasema tuko na mbunge.

David Kamar: *Mito ano chichoto?*

Translator: Yuko wapi?

David Kamar: *Kandoindet nemokikere....*

Translator: Huyo mbunge ambayo hatumwoni.

David Kamar: *Kikere bichaitnyi kityo...*

Translator: Tunaangalia kichwa tunasema ni mbunge?

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** No, no, we don't want (Inaudible)

David Kamar: *Amache ane kandoindet.*

Translator: Maoni yake anataka mbunge.

David Kamar: *Amukikandoik kikekas ngal...*

Translator: Kwa vile sisi ni wachungaji na tulisikia ati (Inaudible)

David Kamar: *Kikekas kelemochei kepchie Chomusiek kobun oeng.*

Translator: Na Wanjemps wanataka tugawanywe katikati.

David Kamar: *Ngotkounoto komosikchinin.*

Translator: Hiyo itakuwa ni hatari (?) kwa sababu (inaudible)

David Kamar: *Kimoche kandoindet nebo Bunge.*

Translator: Tunataka mbunge na ikiwa hatutampata hatutagawanywa katikati.

David Kamar: *Kimoche MP nentyo.*

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Mwambie aweke (inaudible) atuambie maoni mengine.

Translator: *Ne?*

David Kamar: Mbunge.....

David Kamar: *Mbunge kityo.*

Translator: Anasema ni hayo tu.

Com Ahmed Hassan: Christopher Parstenei? Solomon Saidimu? Joseph Keboi?

Joseph Keboi: Asante sana mimi ninaitwa Joseph Kemei.

Com Ahmed Hassan: Kemei ama Kemoi?

Joseph Kemoi: Kemei. Mambo ambayo ningetaka kuwaeleza nyinyi ni machache na nitaenda mbio mbio.

Ya kwanza ni hali ya barabarani. Wazungu waliweka abiria wakuchunga magari yao, wakigonga mbuzi, ama ng'ombe hawalipwi. Na hiyo sasa yeye alikuwa ameweuka hiyo (?) halafu achukue mali ya Mwfrika kama anataka. Kwa hivyo saa hi kama sisi wenyewe kweli tumebadilisha tunataka hiyo iwe sawa. Gari na maji yawe sawa, even.

La pili, Chairman wa County Council achaguliwe na wananchi. Isiwe atachaguliwa na ma Councillors watu mmoja mmoja. Na hata mayor achaguliwe na wananchi. Machiefs wachaguliwe na wananchi kwa maana iko machief wwengine wanachapa wananchi sana na wanasema wataenda wapi. Na tunataka wakae tu na wachaguliwe na wananchi na wakae miaka mitano; halafu wapige tena kura na kama ni mzuri arudishwe.

Sote tunataka iwekwe kura ya maoni kuwania Ubunge, mayor, chairman wa County Council, na ma-Councillors. Kama Councillors, chiefs au mbunge analala, kuwe kunapatikana mahali ambapo pa kumrudisha yeye. Isiwe tu mtu anakaa mpaka anawachokesha wananchi, hakuna mahali anaenda.

Lingine, constituency ya Njmps, tunataka kuwaambia nyinyi mjue ya kwamba iko kwa roho ya kila mmoja wetu. Msione ya kwamba ni watu wachache ambao wanapendekeza jambo hili. Na tuchukuliwe kama iko mtu ambaye tunakataa. Kwa maana wakati tulikuwa tunapanga, mwaka jana mwezi wa kumi na moja, tulikuwa tumeungana tukiwa kama community ya Njmps, na tulisema ya kwamba tunataka kumwona mzee. Mwezi wa kumi na moja tarehe ishirini na nne. Viongozi walikuja huko wa districts na tuliwaomba tunataka kumwona mbunge wetu. Tukaambiwa hawezi kupita siku kuu bila kumwona yeye, m jitayarische vya kutosha. Lakini kwa njia ambayo iko katikati, ilituletea hasara sana, mpaka tumekaa tangu tarehe ile tulipoamua kwenda Nairobi; kwa kukosa namna ya kuingia mlango wa State House (inaudible). Lakini tulikosa kwa maana hakuna namna. Hata kama wewe uko karibu, hata kama tunapiga mlango wake. Miezi nne hakuna kupanda. Ndio sasa tunasema hao viongozi ambao wako katikati yetu na mzee wametutesa ya kutosha, na ndio sasa tunasema Rais wa nchi akae na asiwe mbunge, kwa maana tunaona ya kwamba hawezi kufanya kazi yake vizuri.

Na tunesema tunataka constituency na hatujakataa mzee (?) ametusaidia (?). Lakini nafasi ni ya kuwalilisha sisi kama m jumbe ndio nafasi hiyo inakaa peke yake.

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Bwana Kemei hiyo point tunaifahamu sana, enda kwa nyingine ikiwa uko nayo.

Joseph Kemoi: Lingine ni kuwa elimu ilipwe na Serikali, badala ya kuongeza mishahara ya wafanyakazi, lazima ikomeshe hiyo

halafu iangalie watoto kutoka Form I, mpaka university. Hiyo iangaliwe kwa maana hivyo ndio anatusaidia kuliko kusaidia mtu mmoja. Kuongezea mtu mmoja mmoja na watu wengine wanateseka. Isimame hapo halafu ilipe elimu ya bure kutoka Form I mpaka Form IV.

Lingine ambalo ningependa kuongezea halafu nimalize ni mambo ya wafungwa. Wale ambao wanafanya makosa madogo madogo, katika kila location warudishwe waende kufanya kazi katika location hiyo (inaudible) wafanye kazi ya shule na wapatiwe hata mishahara na afande na wafanye kazi huko kuliko kwenda kufanya (?) kwa nyumba ya Serikali huko (Inaudible) amekuja huko kulete maendeleo.

Inginge (?) angechaguliwa na Serikali kwa maana ni hawa wanafanya kazi zaidi kuliko assistant chiefs, machiefs na ninafikisha hapo, Mungu awabariki.

Com Ahmed Hassan: Asante sana. Joseph Chebii? Councillor Anne Chebol?

Cllr Chebol: Asante sana ma-Commissioners. Nitachukua nafasi hii kuwashukuru kwa kututembelwea sisi katika wilaya ya Baringo katika tarafa ya Marigat. Neno la kwanza kabisa ambalo ningependa kuzungumzia ni kuhusu Serikali ya mitaa, kwa kuwa niko katika sehemu hiyo.

La kwanza ni mayor na mwenyekiti wa baraza la wilaya. Ninapendekeza wachaguliwe na wananchi, moja kwa moja, ili kukatisha wale power brokers ambao wanaingilia katikati, na kupendekeza ambao watafaa interests zao. Na baada ya kuchaguliwa kwa miaka mitano, huyo chairman ama mayor, achunguzwe kwa kipindi cha miaka mitano.

Tatu, local authority ninapendekeza ipewe mamlaka ya kujisimamia, kwa sababu saa hii kazi ambayo inaandikwa katika any Council, kuna job group 1 mpaka job group 9, hiyo inaenda kwa Public Service Commission ambayo imekuwa ni tisho sana kwa Council. Tuko na watu qualified, lakini wakifika Nairobi kwenda kwa interview, watu wanampitisha njia nyingine. Tuko na clerks ambao wamekuwa active miaka mingi na treasurers. Also in every Council in Rift Valley, tuko na clerks ambao ni active (?) in every where and they have qualifications. Kwa hivyo ninapendekeza local authorities ijisimamie, kuandika wafanyikazi wote wa all job groups.

Nne, elimu ambayo wengi wamezungumzia, ninaonelea ya kwamba mtu ambaye anapaswa kuwa diwan ni yule ambaye anayeweza kusoma na kuandika vizuri. La tano, mishahara na marupurupu ya madiwani izungumziwe na tume moja, pamoja na ile ya mishahara ya wabunge kwa kuwa bunge saa hii wanaelekea millioni, moja na Councillor sisi tunashika elfu saba, na yule mtu anawatumikia wananchi ni Diwani.

Sita, jambo ambalo linaitwa nominated Councillors liwe ni jambo la kusahaulika milele katika nchi ya Kenya. Kwa sababu

baada ya mimi kumshinda mwenzangu kwa kuwa ye ye alikuwa rafiki ya power brokers anakuwa nominated, ili ku-frustrate efforts ya moani ya wananchi ambayo ni ya Councillor elect.

Saba, waziri wa local Government kufunga baraza lolote, ninaonelea kwamba ni upuzi mtupu. Maoni yangu iwe tu ni rais peke yake ambaye ana mamlaka ya kuvunja local authority yote, any Council ambayo ime mess. (?)

Kuhusu mambo ya ranching, kuna nyang'au ambaye anaitwa group ranch hapa kwetu, hiyo ni chama ya group ranch ya sehemu inayoitwa Sabaot ama Marigat mahali tunakaa. Mimi ni Councillor wa hapa na hapa hapa ni group ranch. Tuliandikishwa majina na majina yakapelekwa Nairobi, na ndio tukaambiwa we are supposed to pay Kshs 3million ili ardhi igawanywe na hakuna hata hela moja (?) tulipata kwa group ranch, hiyo sehemu ya Serikali ya group ranch. Kwa hivyo group ranch iende milele, hatutaki kusikia mambo ya group ranch.

Lingine ni mambo ya irrigation schemes. Irrigation schemes katika Kenya, wakulima wanakuwa tenants. Hii ni ajabu na sio ajabu sana kwa sababu ni sheria ile ya ukoloni. Kwa hivyo tunamshukuru mheshimiwa Rais kwa hili jambo la akiba. Na hata ninataka niseme ya kwamba ninapendekeza muda wa kutosha upewe Katiba. Kwa sababu kuna mambo mengi ambayo tungetaka mrudi Marigat tena tuwaeleze.

Kuwa tenant, baba yangu anakuwa tenant, mimi ninakuwa tenant, mtoto wangu anakuwa tenant, mjukuu atakuwa tenant, na hata kijukuu na hata kilembwe na hata kilembwekeza na hiyo ni aibu. Kwa hivyo mambo ya tenants ninaomba itupiliwe mbali, isahaulike na iwe ndoto.

Mambo ya uridhi wa ardhi, iwe ni mtu binafsi aridhi ardhi. Katika ile mambo ya ardhi Commissioner of Lands anapeana plot katika Marigat hapa, acre kumi. Na hiyo acre kumi inapewa yule mtu ambaye ako na plot everywhere katika town hii, na katika other big towns in Kenya. Anaongezewa acre, kumi, kumi, kumi! Na yule mwenyeji hata akipewa 50X100 angetaka kujenga ninambiwa maplots isimamishwe. Kwa hivyo hayo mambo ya plots (?) tunaomba tuongezewe mali, mambo ianze bottom top kwa mambo ya ardhi. County Council ama municipal council ipewe mamalaka ya kutosha.

Lingine ni mambo ya mahakama. Mambo ya mahakama, ninaona ya kwamba hatia na pesa, basi waswahilli husema 'asiye na lake aelekee jiwe.' Kwa hivyo mambo ya pesa watu wote wameangamia. County Council inapeana plot kwa mtu. Mtu mwingine tumepatia plot raia, mtu fulani anaenda anachukua wakili anampeleka pale kortini, hivyo anaswaga kwa sababu ya toa kitu kidogo. Kwa hivyo ninapendekeza mahakama iwe autonomous, ijisimamie, isiwe chini ya mtu ye yote.

Katika uchaguzi, uchaguzi itakuwa tu bahati mbaya kwa sababu mtu hupiga bibi yake kwa sababu ya mlolongo. Lakini mimi ninasema kama sio mlolongo mimi singekuwa Councillor. Kwa hivyo ninashukuru mheshimiwa Rais kwa kuanzisha mlolongo. Kwa sababu rigging ni order of the day katika mambo ya siri. Kwa hivyo mimi ninaomba hata mahali pengine Ikiingia siri,

ninaomba mlolongo kwangu kwa sababu kura yangu haitaibiwa.

(Laughing from the audience)

Na kuhusu uchaguzi, uchaguzi wa Diwani ,Mbunge na Rais ifanywe siku mmoja kwa sababu uchaguzi wa Diwani ukifanywa leo, mimi nitapiga yule mtu mwingine ambaye anaomba ubunge, na ya ubunge ikifanyika kwanza atakuja kunimaliza mimi ambaye sikumuunga mkono. Kwa hivyo ifanywe one-day, halafu mtu akose mahali pa kupiga. Na katika kugawanya sehemu kama Baringo Central. Tunaomba ya kwamba ikiwa itagawanywa, Baringo Central, wale wanaohusika...

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Jaribu ku-summarize.

Cllr Chebol: Nina summarize. Wale wanahuksika wasigawanye kwa kuangalia ni sehemu zippi ambazo zinaweza kuwafurahisha ili wapate viti. Kwanza wahusishe the stakeholder, and if they don't do so, basi tutawaonyesha ya kwamba kura ni ya mtu sio ya watu.

Katika kumalizia, Provincial Administration. Katika parovincial administration, Chairman wa DDC anatakiwa kuwa Chairman wa County Council ya district hiyo na D.C. awe patron (?) overall na D.D.O awe secretary ikiwezekana. Machief wote wapigiwe kura. Kila chief after ten years, mambo yake yaangaliwe tena.

La mwisho halafu niende niketi na niondoke niende niketi mahali pangu ambapo nimeketi. Mishara na marupurupu ya Councillors ilipwe mahali pamoja na mishahara ya wabunge. Ilipwe na consolidated fund. Thank you very much.

(Clarification) **Com X** (Inaudible)

Cllr Chebol: Group ranch, we don't want group.

Com Mohammed Sawzuri: You don't want group ranch?

Cllr Chebol: Ehe?

Com Nancy Baraza: (inaudible) what about (?)

Cllr Chebol: (?) hiyo ni kamili kwa sababu iko chini ya Count Council.

Com Nancy Baraza: Niiwache hivyo hivyo?

Cllr Chebol: Ikae Councillor namna hiyo kwa sababu County Council inachangia raia lakini group ranches hakuna mtu inachangia.

Com Nancy Baraza: Hapa Baringo bado mnapiga kura kwa mlolongo?

Cllr Chebol: Mlolongo tunapiga kwa KANU kwa sababu ndio njia mzuri.

Com Nancy Baraza: Kwa party au...

Cllr Chebol: Kwa KANU nomination lakini kwa kura ile kubwa ni siri. Thank you very much.

Com Mohammed Swazuri: Wacha tupatie nafasi hii kwa kiongozi wa KANU chairman Bwana Hosea Kiplagat
(inaudible).

Hosea Kiplagat: Thank you very much commissioners. I don't know whether it is since I came from another (?)
same function (?) like this one, I don't know whether to (?) or to say a few words...

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** (Inaudible)

Hosea Kiplagat: I think mine is the (?) summary because I had presented my points there. I would not want to
(?) some of the things which being said here
(inaudible) and I do believe that this is a Constitution we are not patronizing.

On the side of the mlolongo I believe this is only a capacity and we think the manifesto of the KANU party will
(inaudible) whether mlolongo or by secret ballot (inaudible). Some of you think it is
bit a because mainly some people may not have understood but I may have to name one point which I did not point out on the
other side.

On the Section 2A which (?) expands to the parliament (?) Of the president. but I just
want to suggest that maybe I gave only to the president. if it is more than four times, you are (inaudible).
And after that the president I think it is of my view that the president should also be elected nationally not on the constituency
level. And on those days... that remains either a president, I want to clarify, if after the fourth year the president is
(inaudible) then he should be free to go back to either a constituency (Inaudible) as a Member
of Parliament then no problem. I do not wish to (?) a president who is elected four times, we should not

go by the (inaudible). Because I do not see why we talk of (?) doing things. Considering the freedom and wish of the people there should not be an inhibition on the (?)

(inaudible) has been talk a lot on the other side of Kabarnet and as (?) my views (inaudible). Thank you very much.

Com Ahmed Hassan: Thank you very much. (Inaudible). Joseph (?) amekuja? (Inaudible)

Chepchumba: Asante sana. yangu nitasema kuhusu upande wa kazi. Inaonekana kwa upande wa kuandika kazi...

(Interjection) **Com X:** (Inaudible)

Chepchumba: Inaonekana kwa upande wa kuandika kazi ni shida kwa sababu watu wametumia kuhongana. Kama huna kitu hawawezi kukuandika kazi. Hata kama umesoma namna gani, huwezi kupata kazi. Sasa ningeomba Serikali itoe sheria kuhusu jambo hilo, kwa sababu raia mwema anaweza kuumia. Kwa sababu unaweka pesa macho yako kusoma na baadaye huwezi kupata kazi. So ningeomba Serikali iangalie juu ya jambo hilo.

Ya pili ni masomo kutoka kwa Primary mpaka Secondary, Serikali iangalie itoe masomo ya bure. Kwa sababu watoto wengi wanaweza kukaa bila kusoma, kwa sababu hakuna uwezo wowote na kwa university ilipwe.

La tatu ni kuhusu hospitali. Ningependa Serikali iangalie upande wa hospitali kwa sababu watu wengi hawana pesa. Serikali itoe matibabu ya bure kwa hospitali. Ni hayo nilikuwa nayo, asante sana.

Com Ahmed Hassan: Asante sana Bwana Chepchumba (inaudible). Zakayo Loriko. Zakayo?

Zakayo Loriko: Kwanza ninashukuru kwa vile mlikuja hapa mkaleta (?) kwa sababu tangu (inaudible) iko hapa Marigat. Mimi ninaitwa Zakayo Loriko, sijui linaandikwa namna gani sijui ninasema aje Loriko.

Com Ahmed Hassan: Zakayo Loriko?

Zakayo Loriko: Ninaitwa Zakayo Loriko.

Com Ahmed Hassan: L o r i k o?

Zakayo Loriko: Loriko. Loriko ni nyororo.

(inaudible) (*Laughing from the audience*) Basi maoni

yangu mimi ninaogopa kama utapeleka huko mbele kwa sababu unajua kila mtu yuko na tofauti ya maongezi yake, vile utaongea, niongee maneno mengine ninasema kila siku...

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Hakuna shida mzee endelea tu.

Zakayo Loriko: Kila siku iko mvinyo ninachapa mpaka ninakosa mahali ya kuweka. Basi mara ya kwanza maoni yangu ni kuhusu maneno ya hospitali. Hospitali hii yetu ya Marigat iko na shida kubwa, kwa sababu shida ziko za namna nyingi. Magonjwa ya damu yanamaliza watu hapa Marigat. Kama mtu anakwisha damu, mtu hawesi kufika Kabarnet bila kupoteza maisha. Hata mimi ninapotea mwaka jana (inaudible). Basi ikiwa nyinyi mko na uwezo, mtachukua hilo jukumu ya kututafutia hapa Marigat hospitali ya maana. Kama mtu (inaudible) tunapata ana ugonjwa wa damu kutoka (inaudible) huwezi kufika Marigat tena hapa kwa sababu utakufia njiani kwa sababu damu inamalizika na upopo huu ambaa unavuma. Upopo unakunywa damu ya mtu. (*Laughing from the audience*)

Maneno yangu mengine, mimi mtaona vile mimi ninasema (?) kwa sababu (inaudible) iko Tugen, na iko Pokot hapa. Na hiyo kabilia (Inaudible) halafu je mimi ni Turkana, kwa nini hapana hesabu mimi (inaudible)? (*Laughing from the audience*) Kwa sababu wakati Pokot walipigana na bibi wote walipigana. Kwanza mimi nilipigana zaidi hata vita vya juzi ambayo ilikuwa ni kufa na kupona (inaudible). Kwa nini mimi bado sijasikia jina langu (inaudible) (*Laughing from the audience*) na mimi ni mtu wa Kenya. Kama nchi ya watu wote ni kitu gani ambayo haijaleta jina langu? Hiyo ni ugonjwa, tabia mbaya. (*Laughing from the audience*)

Jambo la tatu

(inaudible) sasa hiyo

(?) ni ya nani? Ni ya Kenya gani?

Kwa hivyo...

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:**

(inaudible) iko Njemps, iko Tugen, Pokot na Turkana.

Zakayo Loriko: Ndio, mimi ninataka kufanya hivyo. (*Laughing from the audience*). Sasa kwa hivyo iko jina kubwa

(?) kwa Marigat kwa sababu hata (inaudible) iko wale hakuna masomo na

(inaudible) kwa sababu hata wale wako na (inaudible) unashinda na pesa kwa sababu pesa hakuna (inaudible). Mtu kama ng'ombe zangu ninauza mbili saa zingine mbili au tatu zinabaki, iko na watoto ninakamua halafu hauna nini? Utauza nini? Unataka sasa mimi ni (?) tunataka sasa watafute namana ya kuelewa zaidi shida za watu.

Com Ahmed Hassan: David Kigen.

David Kigen: Asante. Jina langu ni David Kigen, mkaazi wa hapa Marigat. Yangu ningependa kuchangia, ni kama maoni. Kile kitu ningesema na ninazidi kusema kuna vitu vingi ambayo mbeleni tulikuwa tunatumia na hata saa hii tunatumia.

Maoni ya kwanza sisi ni watu wamila, na mila zetu tunasikia kama mtu akizaliwa kulikuwa na mila fulani na tunataka tujue ziko namna gani. Sisi kwanzia zamani ni watu hupasisha wasichana tohara na ukiona tangu mbeleni ni wale walianza mbeleni walikuwa wanajua, kwa sababu kulikuwa na sababu mingi. Ya kwanza ilikuwa msichana akitahirishwa baadaye anakuja kuolewa, na anakuwa na unyenyekevu na anajua jinsi ya kuchunga bwana. Na tangu siku hiyo ni mwaka wa 1982 mwezi wa sita, hiyo maneno yakasemekana hiyo imekataliwa na tukaona. Mbeleni ilikuwa wasichana hutahiriwa na baada ya kutoka jandoni unaona wanaume wanakuja kuingia kila nyumba ile wasichana wanachaguliwa.

(Interjection) **Com Nancy Baraza:** Hatusikii vizuri, weka microphone mbele usitoanishe mdomo rudia hayo maneno ulisema.

David Kigen: Nilisema mbeleni wasichana walikuwa wanatahiri na baada ya kutoka jandoni wanaolewa haraka. Na kutoka siku hiyo, siku ile (?) unawaoana wasichana wamekuwa shida, wanatangatanga na hawaelewi. Hiyo ndio tulikuja kuona itakuja kukatazwa. Na hiyo mila ilikuwa ni ya mbeleni na hiyo tukanona vile tunataka...

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Kwa hivyo unataka nini? (inaudible) Toa pendekezo.

David Kigen: Nitatoa pendekezo. Sasa mimi ninaonelea mambo hayo yangerudi ili... kwa sababu mambo haya yakukatazwa ni mila ya nyumba ingine. Mila ya nyumba yetu ni ya nyumba yetu. Hiyo habari ya kutolea kwa nyumba nyingine na kuingizwa kwa nyumba nyingine haistahili. Maoni mengine ningependa hiyo kama (?) irudishwe, tufanye arusi.

Com Ahmed Hassan: Unajua iko sheria ya watoto inasema ukifanyia msichana tohara hiyo ni hatia, (?)

David Kigen: Iko namna hiyo, lakini inategemea mtu ambaye anapenda. Inastahili kutegema mtu anavyopenda. Lingine, saa hii iko mtu ambaye anaweza kuingia kwa bar tukisema habari ya vinywaji. Mtu ambaye anajiweza anaingia kwa bar, anakunywa. Na kuna mwingine hajiwezi, kwa hivyo pombe yake haina tofauti na ule uji wa kienyeji. Na hata yeye (?) na yeye apae kitu kidogo. Sasa tungependa nao watu wale hawajiwezi wapate kujiburudisha na kinywaji ya kienyeji.

Lingine kwa sababu ikitsemekana habari ya chang'aa ningependa hiyo kitu itupiliwe mbali kabisa. Lakini hii chai ya wazee ile... (*Laughing from the audience*) inaitwa millet, ile inaitwa uji tupate. Na kwa sababu busaa... kuna wale wanajiweza, wanaenda kwa bar na wengine wale hawajiwezi wapate kidogo. Ni hayo tu nilikuwa nayo, asante.

(*Laughing from the audience*)

Com Nancy Baraza: Ninataka kukuuliza swali. Mambo ya kutahirisha kwa hospitali. Msichana akitahirishwa sasa anaolewa, mpaka aolewe...

David Kigen: Aolewe, ataolewa.

Com Nancy Baraza: Na siku hizi there was a time (inaudible) hawaolewi watu wanawakataa au nini kwa sababu hatujaelewa vizuri ni nini.

David Kigen: Ndipo tunaona wasichana enyewe wakati walipokataliwa kuenda hiyo arusi, hiyo college kwa sababu hiyo ni college (*Laughing from the audience*). Hiyo ni college ya watu. Ikiwa ulisoma ama hukusoma hiyo ni college ya kinyumbani, na hiyo college ndio inafunza watu tabia mzuri, wale hawakusoma. Hata ingalao umesoma, lakini kuna maneno mengine ya kienyeji ambaye hata kama umesoma hutajua iko namna gani. Na tuliona (?) hata mtu akitaka huwezi kuja kwangu ukitaka msichana unauliza (?). Unauliza hata huyo msichana kabla hatujaongea kuhusu mali yake. Ameenda college ama bado?

(*Laughing from the audience*)

Com Nancy Baraza: Iko swali lingine hata mimi nimekaa hapa watu wanasema mnataka muelimishwe mpate masomo kama Wakenya wengine, na wasichana wameacha shule. Na wewe (?) college (inaudible) juu ya ng'ombe, watasoma namna gani ndio wawe kama Wakenya wengine?

David Kigen: Watasoma hata saa hii huwezi kukosa mtu ambaye ameenda university na ameenda hiyo college.

(*Laughing from the audience*)

Kendagor Kisire: Asante sana Commissioners. Yangu ni maneno mawili tu pekee yake. Jina langu ni Kendagor Chesire (?). Maoni yangu ya kwanza, ingawa wengine wameshasema, Chairman wa County Council wachaguliwe na wananchi wenywewe.

La pili kutoka hapo hapo, wakati tunafanya development yule alikuwa kwa D.C yaani chairman yeze apewe mamlaka awe chairman wa kutekeleza mambo ya wananchi. Pia maoni mengine, wakati mwangi ukichaguliwa na kupewa na ni mlevi tutakuja kugongana nyumbani, na maendeleo tunasoma mpaka yeze anaenda retire ama miaka mitano ikiisha. Tunataka kuona sasa wale wamechaguliwa watekeleze mambo ya wananchi kuondoa umaskini kwa wananchi. Kwa sababu tunataka wakati tunaona yule ameendelea kama tunataka kumrudisha kuchukua miaka mitano mingine, kwa sababu ya kutekeleza wananchi kazi ndio tunataka.

Tena mambo mengine, hii pesa kwa sababu imekwisha semekana tunatakikana kulipa pesa ya Councillors kutoka kwa account ile inalia wabunge. Ile pesa tunatozwa ya ushuru, pesa hizo zitengenezee wananchi mabarabara, mashule. Pia ilipe waalimu wa nursery school. Waalimu wa nursery school walipwe kutoka kwa pesa za wananchi ambao wanafanya katika County Council.

La mwisho, iko wezi ambao waniba mbuzi au ng'ombe ya watu halafu wanakuja kukuuzia na wakati ukishanunua pengine ukipatikana nayo ukisema uliuziwa na mwagine, wansema wewe unasaadia wizi. Kwa nini Serikali hawamfuati yule ambaye aliiza wale ng'ombe wa kuibwa? Kwa nini wanataka kuumiza mwenye kununua? Angejuaje? Hicho kitu kinahitaji kukataliwa kabisa katika Katiba (?)

Basi kwa hivyo ningependelea kwa wale machief ambao wanaandikwa, ama wanafanya interview katika Serikali wachaguliwe na wananchi, lakini wakati D.C amewakamata yeze anakaa mpaka wakati inamaliza miaka tano, sio ati mwananchama anachaguliwa tena kama Councillor. Kwa hivyo ningependelea namna hiyo kwa sababu tumekuwa tunachaguliwa watu wengine wa kuja kuumiza wengine, hapo hawajui hata mimi mwenyewe nilipita njia hiyo. Mimi nilifanya kazi ya assistant chief miaka ishirini. Lakini iko kazi nyingine wakati mwagine sisi tukiona haifanywi hakika hata mimi wakati mwagine nilitoka kwa kazi hiyo kwa kuona mambo sio tamu sana. Mambo ni mbaya kuchungakwake kwa sababu siku za mwisho nyumba yako itatikisika. Kwa hivyo sasa kila mtu achunge maisha ya kwake kwa sababu (?) ndio itakuja kukatakatwa. Kwa hayo machache ninasema asante.

Com Ahmed Hassan: Haya nenda sign kwa kile kitabu. Chesire (?) kama hayuko Mary Komet? Okay Toroitich Chergot? Joseph Motogoi? Patrick Koko? Ni wewe?

Patrick Koko: Asante sana kwa Commission na kwa wananchi wa Marigat kwa jumla. Mimi nikoo na furaha kubwa siku ya leo kwa sababu ya hii kazi vile mliitayarisha kwa sababu tulitumaini tutafika siku kama ya leo. Kwa hivyo tunawakaribisha Marigat ili tuweze kubadilisha hii Katiba kwa pamoja.

Kwanza mimi ninataka kurekebisha Katiba. Kwanza ninataka kurekebisha upande wa desturi kwa sababu kama tunarekebisha, tunarekebisha desturi. Mwananchi ama mtu yejote mahali alipo hatuwezi kusimama kama... kama hii nyumba

haiwezi kusimama kama hakuna foundation. Mimi ninashangaa sana kama tutarekebisha kile kitu hakina foundation. Kama tutarekebisha Katiba ile haina foundation, tunarekebisha bure. Mimi mwenyewe maoni yangu ni kusema hiyo tuvuke tuende nyingine. Lakini kama tuko na foundation ya Katiba, nitaingina na nitauliza Mkenya mwengine aingie ili turekebishe, kwa sababu ya... we are dealing with life yaani, tunarekebisha maisha ya kesho, sio ya saa hii. Na kama ni maisha ya kesho, mimi ninarekebisia wale watoto wangu na mimi nitakuwa wapi?

(Interjection) **Com Mohammed Swazuri:** Which foundation are you talking about?

Patrick Koko: Desturi, culture.

Com Mohammed Swazuri: (inaudible) to continue or to be ...

Patrick Koko: To be amended, yaani turudishiwe desturi ile yetu tulikuwa nayo. That is what I mean by foundation. Kwa sababu nimeona kama tungkuwa na foundation, nafikiri hatunge kaa hapa, ama mahali pengine.

Pili, ninakuja kurekebisha sasa tabia ya mwananchi sasa. Kwa sababu tunarekebisha kitu kimoja. Labda nikiulizwa mimi kama ningelizwa tunarekebisha nani atanufaika? Ni mimi, sio mtu mwengine. Sasa mimi sitarekebisha Katiba pekee yangu nitarekebisia Wakenya wote. Kwa sababu nikirekebisha Katiba ya kwangu nitakuwa ninajipenda mimi mwenyewe. Kwa hivyo mimi ninaongea jumla Wakenya wote. Kama tutarekebisha, turekebishe kile kitu amacho kitaingia kwa 41 tribes of Kenya not one tribe. I am talking of 41 tribes of Kenya. Hiyo sasa ninapita ninaingia three.

La tatu ninaongea juu ya misaada. Tumekuwa tukitegemea misaada kwa wakati mrefu na ni vizuri. Mara kwa mara nilikuwa ninaona nikiomba sikuwa na maendeleo yoyote. Nilikuwa ninaomba, ninapatiwa ninakula inaisha ninarudia tena.

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** (inaudible)

Patrick Koko: Sasa natumai tungeachiwa sisi Wakenya tuendelee hivyo. Ninaona misaada kama imeturudisha nyuma sana. Ya mne, ninafikiri ndio ya mwisho. Sitaongea juu ya uchaguzi kwa sababu ile nilikuwa nayo, nilikuwa nimetayarisha ni hiyo. Sasa ya uchaguzi hiyo ni ya wengine. Kwa hivyo ninashukuru sana kwa hayo yote. Karibuni.

Com Ahmed Hassan: Asante. (inaudible) Kiptoo Kimeto? Kama hayuko, Wilson Kireng. Nakuona uko na written memorandum, please do not read it word for word.

Wilson Kireng: Honourable Commissioners...

(Interjection) **Com Ahmed Hassan:** Tell us your name

